SportPesa
TZS. 1,042,431,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SERIKALI** yavuna bilioni 540/- toka mashirika ya umma




Nipashe
Jumamosi Machi 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580889
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# MBOWE: NIMESAMEHE



Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe

**ASEMA** hana kinyongo na 'wabaya wake', abadili gia angani suala la Katiba Mpya, awakana Mdee na wenzake...*Endelea ukurasa 2*

# MWAKA MMOJA

## MAMBO YALIYOMPAISHA SAMIA

- Demokrasia
- Uhuru vyombo vya habari
- Mapambano UVIKO- 19
- Usawa wa Kijinsia
- Diplomasia
- Usalama wa raia
- Ujenzi Miundombinu
- Huduma za Jamii
- Matumaini Watumishi
- Ukuaji wa uchumi
- Utawala Bora
- Mabadiliko ya viongozi



UKURASA 4

# CCM yatangaza kiama viongozi wanaofanya kazi kwa mazoea

UKURASA 2

MICHEZO YANGA, KMC FC MAWINDONI UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya chama hicho, katika utekelezaji wa ahadi zake chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe asema amewasamehe wote

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amefunguka na kusema amewasamehe wote waliomfanyia mabaya.

Mbowe alisema hayo jana zikiwa zimepita takriban wiki mbili tangu Mahakama Kuu ya Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kumwachia huru baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kudai hana nia ya kuendelea na kesi iliyokuwa ikimkabili kwa tuhuma za ugaidi.

Alisema ametoka gerezani akiwa na roho nyeupe na hana kinyongo na mtu yeyote, huku akiwataka wanachama wa CHADEMA nchini nao kutokuwa na visasi bali waendelee kufanya siasa.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maamuzi ya Kamati Kuu ya CHADEMA iliyokutana hivi karibuni.

"Nimesema na ninasema tena, ninatangaza msamaha kwa yeyote aliyefikiri amenifanyia baya. Sina chuki wala kisasi. Nawaomba wanaCHADEMA wenzangu tusiwe na chuki na mtu yeyote katika mapambano haya.

"Mapambano haya ni kupigania ustawi wa watu. Hatuwezi kuutafuta ustawi wa watu wakati tukiwa na kisasi. Kisasi si utamaduni wa CHADEMA wala wa Mbowe. Nimetoka na roho nyeupe kabisa nikiwa tayari kuendeleza mapambano ya kisiasa" alisema.

**ALICHOTETA NA RAIS**

Pamoja na mambo mengine, Mbowe alieleza kile alichozungumza na Rais Samia Suluhu Hassan muda mfupi baada ya mahakama kumwachia huru.

Alisema alifanya mazungumzo katika mambo mengi na Rais Samia ikiwamo kujadili njia bora ya kutafuta amani na suluhisho katika kufanya siasa.

"Jambo la kwanza tulikubaliana tuache kuzungumzia neno amani, amani, amani. Tulikubaliana tuzungumzie neno haki. Jambo la pili, nilimweleza kwamba CHADEMA ni chama kikuu cha upinzani nchini, hivyo maridhiano yoyote yanayofanywa ndani ya taifa hayawezi kufanyika pasipo kukishirikisha CHADEMA," alisema.

"CHADEMA kipo kuanzia ngazi ya kata, kitongoji, kijiji hadi mtaa, hivyo kukitoa ni jambo ambalo haliwezekani. Jambo la tatu tulizungumza na kukubaliana ni kwamba kila upande ujenge imani kwa mwenzake, tusiishi kwa hofu," aliongeza.

**SAKATA LA KINA MDEE**

Kuhusu wabunge 19 wa viti maalumu walioko bungeni, wakiongozwa na Halima Mdee wanaodaiwa kuwa ni wa CHADEMA, Mbowe alisema chama hakijawahi kuteua wabunge wowote.

Alisema Spika wa Bunge aliandikiwa barua na anajua wabunge hao si halali kwa kuwa hawakuteuliwa na chama hicho.

Mbowe alisema Baraza Kuu la CHADEMA litakaa Aprili 25, mwaka huu, na kama kutakuwa na rufani yoyote kuhusu wabunge hao, itashughulikiwa.

**KATIBA MPYA**

Kuhusu Katiba Mpya, Mbowe alisema mchakato huo ni endelevu, kudumu na hauna kikomo.

Alisema kwa sasa CHADEMA imeamua kujikita kwenye mazungumzo ya kudai katiba mpya na kwamba endapo itashindikana, itatafutwa njia nyingine.

Kadhalika, Mbowe alisema CHADEMA hakitashiriki mkutano wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) pamoja na kongamano linalotarajiwa kufanyika Machi 30 mwaka huu jijini Dodoma.

"Machi 21 nimeambiwa kuna kikao cha TCD, CHADEMA tulikubaliana hatutashiriki kwa kuwa hatuna wabunge hadi hali hii itakapobadilika," alisema Mbowe.

Kuhusu kongamano la TCD linalotarajiwa kufanyika Machi 30 na 31, mwaka huu, kwa lengo la kutafuta maridhiano ya kisiasa, Mbowe alisema pia CHADEMA haitashiriki.

# CCM yawatangazia kiama viongozi goigoi

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema hakitawavumilia viongozi watakaoshindwa kuendana na kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuliletea taifa maendeleo.

Pia imesema Rais Samia amefanya maendeleo makubwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake, hivyo kuridhishwa na kasi yake katika kutekeleza ilani ya chama.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia tangu alipoingia madarakani.

Chongolo alisema haiwezekani watu wako kwenye safari moja halafu mwingine afanye hujuma ya kutoboa boti wanayosafiria ili ijae maji. Alisema mtu huyo ni lazima ashushwe kabla ya kuzamisha boti na kusitisha safari ya awamu ya sita.

"Ndiyo maana tumekuwa tukiona mabadiliko yanayofanywa tunaamini wote waliongia wanaendana na kasi ambaye haendi na kasi ataendelea kushushwa njiani. Hiyo ni kawaida, hatuwezi kutembea na boti mtu mwingine yuko 'bize' kutoboa boti ili maji yaingie ndani. Hatuwezi kumwacha maji yajae ili tuzame," alisema.

Chongolo alisema CCM itaendelea kuishauri mamlaka ili kuwashusha wale ambao hawaendani na kasi ambayo Rais anaitaka.

Kuhusu madai kwamba Rais Samia anaongozwa na Rais aliyestaafu, Chongolo alisema mamlaka ya Rais hayawezi kuongozwa na mtu kwa kuwa ile ni taasisi, hivyo ni ngumu kuongozwa kwa 'remote contol'. Alisema mamlaka hiyo ni ya Rais na si ya mtu mwingine.

"Hata mimi ni Katibu Mkuu siwezi kufikiria kuwa naweza kuingilia taasisi ya Rais kufanya ninachotaka. Ile ni taasisi huyo mwenye madaraka makubwa kuliko sisi wenye chama tawala na tunaoongoza nchi, yuko wapi? aje hata atueleze anatumia njia gani kushawishi maslahi yake au chochote anachotaka kufanywa na mamlaka?" alihoji Chongolo.

Alisema hakuna kinachopita bila mamlaka ya Rais kuamua na kama lipo hilo ni tatizo la fikra za mtu na si taasisi na kuwataka wananchi wasiwe na wasiwasi Rais wa nchi na mwenyekiti wa CCM ni msimamizi mkuu na mtendaji mkuu wa kila kinachoendelea katika nchi.

Chongolo alisema nafasi ya CCM katika mwaka mmoja madarakani Watanzania kwa umoja wao wataadhimisha leo ni matokeo ya CCM kupewa ridhaa na Watanzania kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Sote tunajua kuwa katika kutekeleza wajibu na majukumu yake, serikali anayoisimamia na kuiongoza Rais Samia, mbali na kuongozwa na Katiba ya nchi, sheria zinazotungwa na vyombo vya uwakilishi wa wananchi, sera, kanuni na miongozo mbalimbali, pia inatekeleza Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025," alisema.

Chongolo alisema CCM inaposimama kuzungumza kuhusu mafanikio, maendeleo na ustawi wa wananchi na taifa ndani ya mwaka huu mmoja wa Rais Samia madarakani, wanazumgumzia suala ambalo wana wajibu nalo kwa asilimia zote.

Aidha, alisema hali ya kisiasa katika ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 - 2025, hasa katika ibara zilizobebwa na Sura ya Sita, CCM iliwaahidi wananchi kuwa itaimarisha hali ya utulivu wa kisiasa na umoja wa kitaifa nchini, hasa kupitia utoaji haki, utawala bora unaozingatia sheria, kuimarisha misingi ya demokrasia na kutoa madaraka kwa wananchi, ikiwemo uhuru wa kutoa maoni juu ya namna wanavyotaka nchi yao ijitawale.

Alisema lengo la kukutana na makundi mbalimbali ya kijamii ni kuimarisha misingi ya maelewano na kujenga umoja wa kitaifa.

Alitaja makundi ambayo Rais Samia ameshakutana nayo na amekuwa akishirikiana nayo kwa karibu katika uongozi wake ni viongozi wa dini, viongozi wa kimila, ambao pia wamempatia dhamana ya kuwa mkuu wao, 'Chifu Hangaya', walemavu, vijana, wafanyabiashara wadogo wadogo (Wamachinga), Asasi za Kiraia, wanawake, wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), na viongozi wa vyama vya siasa, ama mmoja mmoja au katika makundi.

Aidha, Chongolo alisema ilani ya CCM imetamka serikali kuimarisha viashiria vya ukuaji wa uchumi jambo ambalo CCM inajivunia.

Alisema Rais Samia katika kipindi cha mwaka mmoja amefaya maendeleo makubwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, afya, uchumi, maji, miundombinu, nishati, diplomasia ya uchumi na mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa, michezo na utamaduni na utalii.

# Mbaroni tuhuma mauaji madereva bodaboda

**Na Abdallah Khamis**, MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara, limewakamata watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya madereva wa bodaboda mkoani hapa ikiwa ni mwezi mmoja tangu kutokea kwa mauaji ya mfululizo ya madereva hao na kutupwa katika misitu ya Hiari mkoani hapa.

Waliokamatwa kwa tuhuma hizo ni Badilu Hanongi (29),mkazi wa kijiji cha Mabatini Mtwara, Salum Ally Mauji(24) mfanyabiashara na mkazi wa Tandika, Dar es Salaam na Halfani Namkole(25), mfanyabiashara na mkazi wa Newala mkoani Mtwara.

Kaimu kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi (ACP) Nicodemus Katembo, alisema Februari 15, mwaka huu, baada ya kupatikana miili ya madereva wa bodaboda watatu katika msitu wa Hiari na eneo la Majengo, Jeshi la Polisi liliweka mpango kazi maalum na kupokea taarifa fiche zilizochakatwa kwa kina na kufanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao.

Alisema watuhumiwa wawili walikamatwa katika wilaya ya Tunduru mkoa wa Ruvuma na katika mahojiano ya kina, walikiri kuhusika na mauaji ya madereva wa bodaboda na kwenda kumuuzia pikipiki hizo Halfani Namkole wilayani Newala.

"Tulipowahoji mbinu walizotumia, walisema baada ya kuwakodisha madereva waliowakusudia, waliwaelekeza katika kijiji cha Namagoli na wakifika huko hudondosha kitu chini na dereva anaposimama humshambulia kwa visu, kumfunga kamba miguuni na mikononi na kuwafunga bandeji mdomoni na puani," alisema ACP Katembo.

Alisema watuhumiwa hao wameshafikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mtwara wakituhumiwa kwa mauaji ya madereva hao wa bodaboda.

Februari 15, mwaka huu, madereva wa bodaboda mkoani Mtwara walifanya msako wa pamoja baada ya wenzao watatu kupotea katika mazingira tofauti na katika msako huo walifanikiwa kukuta miili yao ikiwa imetupwa katika msitu wa Hiari.

ACP Katembo aliwataja waliouawa kuwa ni Kelvin Mbale, ambaye mwili wake ulitambuliwa kutokana na kukutwa nguo na viatu vikiwa pembeni ya viungo vyake.

Wengine ni Mohamed Juma, aliyechomwa na kitu chenye ncha kali chini ya sikio upande wa kulia huku kukiwa na dalili za kunyongwa na shingo akiwa amefungwa kamba na Mohamed Juma Mohamed (22) aliyetoweka kijiweni kwao kuanzia Februari 10, mwaka huu.

# Serikali yavuna bil. 540/- mashirika ya umma

**Na Mwandishi Maalumu**, DODOMA

OFISI ya Msajili wa Hazina imekusanya Sh. bilioni 539.39 kutokana na mapato yasiyo ya kodi kati ya Machi 2021 na Februari, mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 105 kutoka kiasi cha Sh bilioni 262.99 kilichokuwa kimekusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita.

Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto alisema hayo jijini Dodoma alipokuwa akielezea mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Alisema makusanyo hayo ambayo ni moja ya majukumu ya Msajili wa Hazina, yamepata ufanisi kutokana na mapato kuimarika mwaka hadi mwaka, hivyo kuongeza mapato yasiyo ya kodi yanayojumuisha gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi na mapato mengineyo.

Ufanisi huo uliotangazwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina inayosimamia taasisi na mashirika ya umma 287, ikijumuisha kampuni na taasisi 40 zinazomilikiwa na serikali kwa hisa chache na taasisi 10 za nje ya nchi, umetokana na usimamizi madhubuti wa serikali na maelekezo thabiti kutoka kwa Rais Samia.

Sambamba na hilo, alisema Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeokoa fedha za umma na mali za Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) zilizowekwa dhamana katika Benki ya Exim Tanzania.

Awali, kampuni hiyo ilishindwa kulipa deni la Dola za Marekani milioni 6.7 na baada ya majadiliano, serikali ililipa Dola milioni 2.7, hivyo kuokoa Dola milioni 4 pamoja na mali za TFC kama maghala na jengo la ofisi vilivyokuwa vimewekwa dhamana.

Pia msajili alisema serikali kupitia ofisi yake, imewezesha Benki ya Maendeleo (TIB DFI) kurejeshewa fedha za madeni ya mikopo iliyokuwa hailipiki iliyotolewa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Kwa mujibu wa msajili, deni la TPDC lilikamilishwa Novemba, 2021 ambapo Dola za Marekani milioni 34.39 zililipwa huku deni la NHC - mpaka kufikia Desemba 31, 2021, NHC ilisharejesha Sh. bilioni 30.16 na deni lililobaki ni Sh. bilioni 17.62 na malipo yanaendelea kufanyika.

Kuhusu deni la TANESCO, alisema mpaka Desemba 31, 2021, shirika lilirejesha Sh. bilioni 29.40 na deni lililobaki sasa ni Sh. bilioni 15.58 na linaendelea kulipwa.

"Malipo ya madeni ya mikopo hii yameiwezesha Benki ya TIB DFI kuimarisha hali yake ya ukwasi na kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake," alisema.

**UPANUZI KILOMBERO**

Akizungumzia upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, alisema serikali kupitia Msajili wa Hazina pamoja na wanahisa wenza (Illovo Group) imeingia makubaliano kutekeleza mradi mkubwa wa upanuzi wa kiwanda kwa gharama ya Sh. bilioni 571.6, sawa na Dola za Marekani milioni 238.5.

Uwekezaji huo, alisema unatarajia kuzalisha tani 144,000 za sukari ambazo zitaongeza uwezo wa kiwanda kuzalisha sukari hadi tani 271,000 kutoka tani 127,000 za sasa.

Msajili pia ameokoa shamba la Mngeta - Kilombero Plantation Limited (KPL) kwa kulinunua kwa Dola za Marekani milioni 7.40 kwa mujibu wa taarifa ya Mthamini Mkuu wa Serikali, shamba la Mngeta lina thamani ya Sh. bilioni 152.19.

"Ni dhahiri kuwa uwekezaji huu ni mkubwa na serikali itapata rudisho thabiti na endelevu" alisema Msajili na kuongeza kuwa Serikali iliamua kukabidhi mali hizi kwa Kampuni ya SUMA JKT ambayo inajishughulisha na vitega uchumi mbalimbali ikiwemo Kilimo cha Biashara, ambapo tayari shughuli za kilimo zimeanza.

PSSSF Public Service Social Security Fund

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma




Mwenyekiti, Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini, Menejimenti, Watumishi na Wanachama wa PSSSF, tunakupongeza

**Mhe. Samia Suluhu Hassan,**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

kwa kutimiza mwaka mmoja wa Serikali unayoiongoza ya Awamu ya Sita. Umefanya mambo mengi mazuri kwa kipindi kifupi, PSSSF tunaahidi kuendelea kutimiza majukumu yetu kwa weledi.

# kaziiendelee

PR&ME - Machi 2022

Leo. Kesho. Pamoja. 0800 110 040 www.psssf.go.tz PSSSF Watumishi_Pension PSSSFTZ

# Mambo yaliyompaisha Samia mwaka mmoja

Na Romana Mallya

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatimiza mwaka mmoja tangu aingie madarakani huku akiwa amefanya mambo mengi ambayo yamempaisha katika kipindi hicho baada ya kuchukua nafasi hiyo kutokana na kifo cha mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Katika kipindi hicho, Rais Samia amefanya mageuzi makubwa katika sekta mbalimbali zikiwamo diplomasia, huduma za jamii, habari, ulinzi, utawala bora na demokrasia.

Katika eneo la diplomasia, Rais Samia ameupiga mwingi kwa sababu amehakikisha nchi inakuwa na ushirikiano na mataifa mengine duniani. Katika kurejesha uhusiano wa kimataifa, alimteua mwanadiplomasia mbobezi, Balozi Liberata Mulamula, kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Baadaye akamteua mbobezi mwingine, Balozi Lazaro Sokoine, kuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo na hakuishia hapo, amefanya uteuzi wa mabalozi kwa kuzingatia masuala ya uhusiano wa kimataifa kuwa unapaswa kufanywa na kuongozwa na watu waliosomea na kukulia katika eneo hilo.

Aidha, amefanya ziara mbalimbali na kutembelewa na marais wa nchi zingine ikiwa ni kiashiria cha uhusiano mzuri na hili limezaa matunda kwa kuwezesha ugeni wa viongozi wa mashirika mbalimbali.

Katika kufanya hivyo, amerejesha uhusiano na mataifa na mashirika mbalimbali, hatua ambayo duniani ikiwamo Benki ya Afrika pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya kiuchumi imewezesha kutiwa saini kwa mikataba mbalimbali na nchi kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Moja ya mikopo hiyo ni ule uliotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wa Sh. trilioni 1,3 kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO- 19. Fedha hizo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile elimu, utalii, afya na miundombinu.



Rais Samia Suluhu Hassan, siku alipokula kiapo cha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 19 mwaka jana.

**HUDUMA ZA JAMII**

Kwa kipindi cha mwaka mmoja, kumekuwa na maendeleo kwenye huduma za jamii kama vile afya, elimu na maji safi na salama.

Wizara ya Afya, kwa mfano imepokea Sh. bilioni 891.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo lengo ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya.

Miradi ya maendeleo ya kipaumbele iliyotekelezwa moja kwa moja na wizara hiyo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali za rufani za mikoa, kanda, hospitali malaum na Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo Sh. bilioni 90.4 zilitolewa.

Katika sekta ya maji, zaidi ya Sh. bilioni 934.3 zimetolewa kutekeleza miradi mbalimbali mijini na vijijini.

Sekta ya kilimo, maeneo matano yameongezewa bajeti ambayo baadhi yake ni utafiti (Sh. bilioni saba hadi Sh. Bilioni 11), uzalishaji mbegu (Sh. Bilioni 5.42 hadi Sh. bilioni 10.58, maofisa ugani (Sh. milioni 603 hadi Sh. bilioni 11.5) na umwagiliaji (Sh. bilioni 17.7 hadi Sh. bilioni 51.48).

**ELIMU**

Sekta ya elimu, wataalam wa elimu na sekta mbalimbali wapo kwenye mchakato wa kuboresha mtaala wa elimu.

Katika kuboresha elimu ya ufundi, seikali imetoa Sh. bilioni 30.84 kwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA) kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya 25 ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu hiyo.

**VYOMBO VYA HABARI**

Katika mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia, nuru ya kuwapo kwa uhuru wa habari imeanza kuonekana baada ya kuitaka Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kuondoa marufuku dhidi ya vyombo vya habari ambavyo vilikuwa vimefungiwa kwa vipindi tofauti. Vyombo hivyo ni pamoja na TV mtandaoni na magazeti manne ya MwanaHALISI, Mseto, Mawio na Tanzania Daima.

Aidha, yamefanyika mabadiliko katika baadhi ya sheria na kanuni ambayo yamegusa maeneo mengine ya uhuru wa wananchi kujieleza na uhuru wa habari.

Pia kuwekwa mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo yanachangia kuongeza ajira kwa vijana sambamba na marekebisho ya kanuni za utangazaji kwa njia ya kidigitali za mwaka 2018 yamefanyika ili matangazo ya televisheni yawafikie wananchi wengi.

**USALAMA WA RAIA**

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya uonevu unaofanywa na baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi ikiwamo tuhuma za kushiriki matukio ya uhalifu, uporaji mali na mahabusu kufia kweye vituo vya polisi pamoja na wananchi kubambikiwa kesi.

Hatua hiyo ilimfanya Rais Samia kutaka chombo hicho kujitafakari juu ya utendaji wake ili kurejesha imani kwa wananchi ambayo imetoweka.

**VITA UFISADI**

Ndani ya mwaka mmoja, wananchi wamemshuhudia Rais Samia alivyofanya mabadiliko makubwa katika taasisi za umma zikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kwa kumwondoa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Deusdedit Kakoko na Shirika la Wakala wa Huduma za meli Tanzania (TASAC).

Lengo la kufanya hivyo ni kutokana na mambo yaliyokuwa yakifanyika ndani ya taasisi hizo ikiwamo ukiukwaji wa kanuni na taratibu za uendeshaji pamoja na ubadhirifu wa mabilioni ya fedha.

Pia alizivunja bodi mbalimbali zikiwamo za TPA na TASAC na Shirika la Posta Tanzania kwa kuwaondoa wenyeviti baada ya kutoridhika na utendaji kazi wao.

Katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri lililofanyika mwanzoni mwa mwezi Januari, mwaka huu, Rais Samia aliwaacha nje aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi .

**KUIMARISHA MASHIRIKA**

Rais pia katika kipindi cha mwaka mmoja, amefanya uteuzi kwenye mashirika ya umma ikiwa ni hatua ya kuzisuka taasisi hizo na kuimarisha utendaji kazi. Katika uteuzi huo, alimteua Nehemia Mchechu kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Peter Ulanga kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Dk. Baghayo Saqware kuwa Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Wengine ni Dk. James Mataragio kuwa Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Masha Mshomba (Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii- NSSF), Erick Hamisi (TPA) na William Erio (Tume ya Ushindani- FCC).

**UVIKO-19**

Ujio wa Rais Samia umeleta mageuzi na mtazamo mpya katika mapambano dhidi ya UVIKO- 19. Tofauti na kabla hajaingia madarakani, Rais Samia alitangaza wazi kwamba UVIKO-19 ipo na kuwataka Watanzania kuchukua hatua mbalimbali kujikinga.

Alikwenda hatua zaidi kwa kukubali chanjo dhidi ya ugonjwa huo ambao umeangamiza mamilioni ya watu duniani. Samia hakutangaza tu chanjo bali alijitokeza kuwa Mtanzania namba moja kuchanja.

Katika kufanya hivyo, aliwahakikishia Watanzania kuwa chanjo hiyo ni salama huku akibainisha kuwa ameamua kujitoa muhanga akizingatia kuwa anabeba dhamana ya kuwaongoza zaidi ya Watanzania milioni 60 kujitosa katika chanjo hiyo.

**DEMOKRASIA**

Baada ya kuingia madarakani wiki chache, Rais Samia alitangaza utayari wake wa kukutana na viongozi wa vyama vya upinzani. Hatua hiyo ililenga kile alichosema kutaka kuleta 'uhuru wa kidemokrasia'.

Ndani ya mwaka mmoja amekutana na viongozi wa vyama hivyo pamoja na wadau wa siasa na kuweka mambo sawa kuhusu masuala ya kidemokrasia. Kwa sasa kuna mambo yaliyofikiwa ikiwamo mapendekezo juu ya namna ya kuendesha siasa.

Aidha, Rais ameagiza kuandaliwa kwa kanuni za kufanywa kwa mikutano ya vyama vya siasa, jambo ambalo linatoa nuru mpya kurejea kwa uhuru wa demokrasia uliokuwa ukilalamikiwa kuwa umeminywa kwa miaka mitano.

Jambo kubwa la kihistoria ni lile la Machi 4, mwaka huu, alipokutana na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Ikulu jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kuachiwa huru katika kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaongeza umiliki hisa kampuni za madini

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imeongeza umiliki wa hisa katika Kampuni ya Madini ya Almasi ya Williamson Diamond kutoka asilimia 25 hadi asilimia 37.

Aidha, hadi Machi, mwaka huu, serikali imetia saini mikataba ya ubia na kumiliki asilimia 16 ya hisa zisizohamishika kwa kampuni tano za madini za Black Rock Mining Limited; Strandline Resources Limited; Petra Diamonds Limited; Nyanzaga Mining Limited na LZ Nickel Limited.

Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, alisema hayo jana wakati akielezea mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha mwaka mmoja ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema vyeti vya umiliki wa hisa vya kampuni za Faru Graphite Corporation, Sota Mining Corporation, Williamson Diamond Limited (Class A & Class B Shares), Nyati Minerals Limited na Tembo Nickel Refining Limited, vilitiwa saini na kukabidhiwa kwa serikali.

Kuhusu mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani, Msajili wa Hazina alisema kumekuwa na mafanikio makubwa katika kutekeleza Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini, Sura 123 kuhusu hisa zisisohamishika za serikali zinazowezesha umiliki.

Ofisi ya Msajili wa Hazina, kutokana na wajibu wake, imewezesha serikali kumiliki hisa katika kampuni za madini zisizopungua asilimia 16 (undilutable 16% Free Carried Interest).

Utekelezaji wa Kifungu hicho cha sheria kuhusu hisa zisizohamishika, umeendelea kuiwezesha serikali kuwa na hisa katika baadhi ya kampuni za madini pamoja na kuongeza umiliki kwenye baadhi ya kampuni katika kipindi kinachoishia Machi, 2022.

Akizungumzia ulipaji wa pensheni kwa wastaafu waliokuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, alisema kuanzia Machi, 2021 hadi Machi, mwaka huu, serikali imelipa Sh bilioni 8.7 kwa wastaafu hao ambao walikuwa hawajaanza kulipwa kiwango cha chini cha pensheni kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Mwaka 2009 na 2015.

Benedicto alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.77 zimetumika kulipa wastaafu 992 wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Sh milioni 798.62 wastaafu 267 wa Shirika la Posta (TPC) na Sh bilioni 6.2 wastaafu 848 wa TTCL.

Aidha, alisema kati ya fedha zote zilizolipwa kwa TTCL, Sh. bilioni 4.77 ni malimbikizo ya nyongeza ya pensheni kwa wastaafu 636 kwa kipindi cha 2009 hadi Februari 2022.

Alisema kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina ikiwa msimamizi mkuu wa uwekezaji wa serikali kwa niaba ya Rais, itaendelea kusimamia kwa karibu utendaji wa mashirika na taasisi za umma ili kuhakikisha kuwa serikali inapata faida ya uwekezaji wake sambamba na kuongezeka kwa mapato yasiyo ya kodi ili kusaidia miradi ya maendeleo kwa faida ya Taifa na wananchi wote kwa ujumla.

## Mwinyi asema Kiswahili kimekuwa daraja kwa masuala ya maendeleo

Na Mwandishi Wetu, ARUSHA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Kiswahili kimekuwa daraja muhimu la kuimarisha uhusiano na utengamano katika maendeleo ya uchumi, biashara, siasa na diplomasia katika ukanda wa Afrika ya Mashariki, Afrika na dunia nzima. Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akifunga Kongamano la Pili la Idhaa za Kiswahili Duniani lililofanyika kwa siku tano, huko katika ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini hapa. Kongamano hilo limeandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 200 likiwa na kaulimbiu "Tasnia ya Habari kwa Maendeleo ya Kiswahili Duniani".

Alisema hali hiyo imechangiwa na jitihada za viongozi wakuu waliopo na waliotangulia katika kuikuza lugha ya Kiswahili na kwamba jitihada za Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, zinaonekana katika kuiendeleza lugha hiyo kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli. Alisema wote hao wameunga mkono jitihada za viongozi wa Tanzania waliotangulia katika kuikuza na kuiendeleza lugha hiyo.

Dk. Mwinyi alisema kutokana na jitihada hizo, Kiswahili kimeendelea kupata mafanikio kwa kuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika kuwekewa siku maalumu na lugha hiyo imepitishwa kuwa miongoni mwa lugha za kazi katika Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Alisema sababu nyingine inayochangia kuongezeka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili ni kutokana na mchango na kuongezeka kwa idadi ya vituo vya redio vinavyotangaza kwa lugha hiyo akiweka bayana kwamba redio zinazotoa matangazo kwa lugha hiyo Tanzania hivi sasa zimefikia 183.

Licha ya ongezeko la idhaa zinazotangaza kwa lugha ya Kiswahili Tanzania, pia alisema kuna ongezeko kubwa la idhaa za nje ya nchi zinazotangaza kwa lugha hiyo adhimu na hadi mwishoni mwa mwaka 2021, zilikuwa takribani 39.

Pia alisema idadi ya vituo vya televisheni nchini vinavyotoa matangazo kwa lugha ya Kiswahili pia imekuwa ikiongezeka kila mara na hadi sasa vimefikia 45 huku magazeti nayo yakiongezeka kutoka sita tu yaliyokuwepo nchini kabla ya Uhuru na hivi sasa kufikia 283.

Alisema kuwa kuna mchango muhimu wa kuongeza wazungumzaji wa Kiswahili kupitia usomaji wa maandiko ya vitabu na makala kadhaa za Isimu na Fasihi ambapo Kamusi za Kiswahili na majarida ya taaluma mbali mbali yameweza kuandaliwa katika kipindi cha baada ya Uhuru na kusaidia sana maendeleo na ukuaji wa Kiswahili hapa Tanzania pamoja na nchi za nje zinazojifunza lugha hii.

"Mafanikio ya kukua kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili hivi sasa tunayashuhudia pia kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Tayari Kampuni ya Microsoft imetayarisha programu za kompyuta kwa ajili ya lugha za Kiafrika kikiwemo Kiswahili," alisema Dk. Mwinyi.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Simba kusajili mapema, wengine igeni

**WAKATI** ikiwa katika kibarua cha mechi za hatua ya makundi kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam tayari imetajwa kuanza mchakato wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao.

Kesho Simba, wawakilishi pekee wa Tanzania na Afrika Mashariki waliobakia kwenye mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), itashuka dimbani Benin kuvaana na Asec Mimosas katika mchezo wa Kundi D.

Asec Mimosas ya Ivory Coast inachezea mechi zake Benin kutokana na viwanja vya nchini kwake kuwa kwenye maboresho ya kuelekea fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Simba ambayo inaonekana imeimarika na ina uzoefu wa kushiriki mashindano ya kimataifa sasa imeanza kufanya michakato yake kwa kuzingatia mahitaji ambayo hukutana nayo kwenye michuano hiyo ya CAF.

Ni kama vile unaweza kusema tayari Simba imeanza kujipambanua na klabu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na namna inavyojiendesha licha ya baadhi kutamba zinafanya shughuli zake kwa weledi.

Kwa kawaida dirisha la usajili huanza baada ya kukamilika msimu na dirisha hilo huhusisha timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championsip (zamani Ligi Daraja la Kwanza), First League (Ligi Daraja la Pili) na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, na hufunguliwa rasmi baada ya kutangazwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Wakati sasa hata dirisha dogo la usajili ambalo hutoa nafasi kwa klabu kuongeza nguvu na kuimarisha vikosi vyake kutokana na mapungufu waliyoyabaini katika mechi za mzunguko wa kwanza ikiwa imemalizika, lakini tayari tunasikia Simba imeshakamilisha baadhi ya usajili wa nyota wake wapya wa kimataifa.

Lakini pia wachezaji wengine wa kigeni wakiwa kwenye hatua nzuri za kukamilisha usajili wa kuja nchini kujiunga na Simba kwa ajili ya msimu ujao, bado klabu nyingine zikiwa zimelala au zinaendelea na mikakati ya kuwania ubingwa huku wengine wakipambana kujinasua kushuka daraja.

Hatua ambayo Simba imefikia, inapaswa kuigwa na timu nyingine kwa ajili ya kuimarisha timu zao kwa maslahi ya kuendelea kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara iwe imara, lakini pia kujiweka tayari kukabiliana na ushindani kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Kitendo cha kuanza mchakato wa usajili mapema na kwa kuangalia wachezaji walioko kwenye ligi kitasaidia kupata nyota wenye uwezo na kutawaepusha kusajili wachezaji wa majaribio ambao kwa kiasi fulani huzigharimu timu kwa kuwasubiri viwango vyao kurejea katika ushindani.

Timu zitakazofanya mchakato wa usajili mapema na kwa utulivu, hakika zitajiweka kwenye nafasi ya kufanya vizuri katika msimu ujao na kuacha kugombania mchezaji mmoja kama ilivyozoeleka.


Jambo zuri huigwa, Yanga, Azam, Namungo, DTB inayofanya vizuri katika Ligi ya Championship na timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara amkeni sasa kwa kuanza kuufikiria msimu ujao na kuacha kufanya usajili wa zimamoto zikiwa zimesalia siku chake, kuanza mazungumzo ya awali na wachezaji ni uamuzi sahihi kwa sababu utatoa nafasi kwa makocha kuwafuatilia ili kuridhishwa na viwango vyao.

Ingawa bado msimu haujamalizika, lakini kwa kiwango kikubwa kila timu imeshafahamu mahitaji yake halisi kuelekea msimu mpya, ni ukweli usiofichika timu itakayokuwa kwenye nafasi ya kufanya vizuri ni ile itakayokuwa ilifanya usajili bora na ilipata maandalizi sahihi wakati wa Pre Season.

Nipashe inazikumbusha timu zote kubadili mfumo wa utendaji wake kazi kwa kubadilika na kufuata mahitaji halisi ya soka la sasa ambapo usajili wa zimamoto kamwe hautawafikisha kwenye mafanikio.

Kama Simba imeanza, basi timu nyingine hazijachelewa, muda unaruhusu kwa kuanza kusaka wachezaji watakaowasaidia na hatimaye itawapunguzia gharama ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha pale ambapo itaonekana mchezaji huyo amekuwa lulu, lakini itaifanya Tanzania kuwa na wawakilishi imara kwenye michuano ya CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## Muda umefika wachezaji kulipwa malimbikizo yao

Na Adam Fungamwango

**SHIRIKISHO** la Soka Tanzania (TFF) limeanza kutoa fomu za leseni kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza) na First League (Ligi Daraja la Pili), kwa ajili ya msimu ujao wa 2022/23.

Fomu hizo zilianza kutolewa Machi 15, mwaka huu na mwisho wa kuchukuliwa na kurejeshwa ni Aprili 25, mwaka huu. Kikubwa zaidi TFF imesisitiza klabu yoyote itakayokuwa inadaiwa na mchezaji haitapatiwa leseni ya ushiriki wa ligi msimu ujao.

Chama cha Wachezaji wa Soka Tanzania (SPUTANZA), kimekuwa cha kwanza kupongeza hatua hiyo, na hii ilitegemewa kwa sababu mara nyingi ndio kimekuwa kimbilio la wachezaji mara wanapoona wanazungushwa kupata stahiki zao.

"Nawapongeza sana TFF kwa kuliona hili, hiki kilikuwa ndio kilio chetu cha muda mrefu, tumepigana sana kuhakikisha kanuni hii iwekwe kwa klabu inapotaka kupewa leseni, leo wamesikia kilio chetu. Ni jambo la kuhuzunisha na kusikitisha kuona mchezaji anaiacha familia yake, anakwenda kukaa kambini kwa muda mrefu na kuitumikia timu kwa nguvu na jasho lake, lakini baadhi yao wamekuwa wakimaliza mikataba yao wanakuwa bado wanadai, pamoja na hayo wanakuwa wanazungushwa kitu ambacho hakipendezi kwenye zama hizi za soka la kulipwa," alisema mwenyekiti wa chama hicho, Mussa Kisoki.

Kwa tangazo hili la TFF, huu sasa ndiyo wakati wa wachezaji kuanza kudai malimbikizo yao na wala si mwingine. Wakisubiri watachelewa.

Nilisikia kuna baadhi ya wachezaji wa klabu kubwa tu za Simba na Yanga wanazidai timu hizo mishahara yao ya tangu mwaka 2004.

Huwa nashangaa kwa nini siku zote hizi hawadai? Ukweli ni kwamba baadhi ya wachezaji wa Kitanzania wanachukulia kama walikuwa wakicheza kwenye klabu hizo kwa kuzisaidia na haikuwa kazi.

Ndio maana wamekuwa hata wakimaliza mikataba yao hawadai, badala yake wananung'unika kichinichini, au linapotokea jambo lolote kwa kumkwaza ndipo wanapofunguka.

Ndiyo maana unaweza kukuta kipindi hiki hakutokuwa na mchezaji wa kwenda kudai fedha zake.

Najua TFF wana orodha ya wachezaji wanaozidai klabu. Inawezekana ndiyo watakazotumia kuzibana klabu hizo, lakini pia wapo wachezaji ambao hawajapeleka malalamiko TFF wala SPUTANZA lakini wana vielelezo vyote, huu ndiyo wakati sasa wa kufanya hivyo ili kupata stahiki zao.

Hakuna klabu itakayokubali kunyimwa leseni na kushindwa kucheza Ligi Kuu msimu ujao eti kwa sababu ya madeni ya wachezaji. Watatafuta popote pale ili wamalize tatizo hilo.

Wasisikilize ahadi na maneno matamu ya viongozi kuwa wasubiri, au kuahidiwa kupewa ofa ya kufundisha timu na nyinginezo.

Tatizo kuna baadhi ya wachezaji wanazidai klabu mbalimbali za Ligi Kuu zikiwamo zile zinazoitwa au kujiita kubwa, lakini viongozi wao ukifika wakati kama huu, wanawasiliana nao na kuwapiga maneno kwa lugha nzuri ya matumaini ya kuwalipa, wakiwataka kukaa kimya kwa ahadi ya kuwalipa baadaye, kuwapa umeneja, au ukocha kwa wale wanaodai kwa muda mrefu.

Kumbe nia ni kupitisha muda wa leseni. Viongozi hao wanapozipata leseni wanaanza kutopokea simu na hapo wachezaji ndipo wanapoibuka na kudai, wakati tayari leseni zimeshatoka na hakuna chochote kitakachowapata.

Kutokana na hilo, wale wachezaji wa zamani wanaozidai timu hizi ambazo bado zipo kwenye Ligi Kuu, Championship na Ligi Daraja la Pili au Ligi Kuu ya Wanawake kwa sasa, ndiyo muda wa kukusanya vielelezo na kuvipeleka TFF kuonyesha madai yao, na hapo hakutokuwa na namna yoyote ile ya kuepuka kutolipwa.

Kitakachokuwepo tu hapo, ni namna gani ya kulipwa, kama ni kukabidhiwa hapo hapo au klabu zitakuwa zinakatwa kwenye mechi zao zitakazokuwa zinacheza. Wakati ni sasa, wachezaji wasikubali ahadi na maneno matamu ya viongozi, watakuja kujuta baadaye zoezi hili litakapomalizika na leseni kuwa mikononi mwa klabu, Hapo wajue kabisa hawatolipwa.

HABARI KITAIFA

# Watu wenye ulemavu waomba kutobaguliwa ujenzi reli kisasa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATU wenye ulemavu mkoani Shinyanga, wameomba kutobaguliwa katika ajira kwenye mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha tano ambacho kinatoka Mwanza hadi Isaka wilayani Kahama.

Mradi huo wa SGR kipande hicho cha tano, umeshaanza kutekelezwa na sasa ujenzi wake uko asilimia 4.5 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024 kwa gharama ya Sh. Trilioni 3.062.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Shinyanga, Richard Mpongo, alisema juzi kuwa watu wenye ulemavu wanapaswa kunufaika na mradi huo wa ujenzi kwa upande wa ajira badala ya kubaguliwa.

Alisema si watu wote wenye ulemavu hawawezi kufanya kazi bali wako wale ambao wana sifa za kupata ajira kwenye mradi huo na kupata kipato cha kuendesha maisha yao pamoja na kujikwamua kiuchumi.

"Tunaomba sana mradi huu wa SGR kipande cha tano, ambacho kinapita katika maeneo mbalimbali hapa Shinyanga, kikitokea Mwanza hadi Isaka wilayani Kahama, watu wenye ulemavu tusibaguliwe kupata ajira kwa sababu kuna kazi ambazo tunaweza kuzifanya na kupata kipato," alisema Mpongo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alipotembelea mradi huo juzi, aliagiza vijana wa maeneo husika ambao wanapitiwa na mradi huo wapewe kipaumbele cha ajira badala ya watu kutoka nje ya maeneo hayo au mikoa jirani.

Alisema utoaji huo wa ajira uzingatie pia usawa wa kijinsia, huku akisisitiza wanawake na watu wenye ulemavu kwa kuwa kuna kazi hazihitaji nguvu ambazo wanaweza kuzifanya, ikiwamo ya ushikaji wa bendera kwa ajili ya kuongoza magari wakati wa ujenzi.

Naibu Meneja wa Mradi wa SGR Kipande cha Tano, Mhandisi Alex Bunzu, alisema walishamwagiza mkandarasi ambaye anatekeleza mradi huo kuajiri na watu wenye ulemavu, kwa kufanya shughuli nyepesi ambazo wana uwezo nazo kulingana na hali zao.

Alisema katika mradi huo wa ujenzi wa kipande cha tano kutoka Mwanza hadi Isaka, wameajiriwa vijana 2,094 na vibarua 859 na kutoa kazi kwa kampuni za ndani 32 na kwamba mradi utakamilika 2024.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja.

# DAWASA yamaliza kero ya maji Chalinze

**Na Joseph Mwendapole**

KERO ya huduma ya maji iliyodumu kwa muda mrefu katika mji wa Chalinze mkoani Pwani, imemalizika baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kukamilisha utekelezaji wa mradi wa Mlandizi - Chalinze - Mboga.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya DAWASA, Jenerali (mstaafu) Davis Mwamunyange, alisema hayo jana wakati wa ziara ya wajumbe wa bodi hiyo kwenye miradi mbalimbali ya maji inayosimamiwa na mamlaka hiyo.

Alisema kuwa mradi wa maji wa Mlandizi-Chalinze-Mboga umesaidia kwa asilimia kubwa kumaliza tatizo la maji kwenye mji wa Chalinze.

"Mradi umekamilika na wakazi wa Chalinze na maeneo jirani wameanza kupata huduma ya majisafi kwa muda wote wa siku. Bodi imetembelea kuona utekelezaji wa mradi, tumejiridhisha na kazi kubwa iliyofanywa na menejimenti, hivyo ni wakati muafaka kwa wananchi kuchangamka kupata huduma ya majisafi kikamilifu," alisema.

Mradi wa maji Mlandizi-Chalinze-Mboga, umetekelezwa kupitia fedha za ndani za zitokanazo na makusanyo ya kila mwezi kiasi cha Sh. bilioni 18.6.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Juni, 2019 kwa lengo la kutoa huduma kwa wakazi wengi wa Chalinze.

Awali, mji wa Chalinze ulikuwa na changamoto kubwa ya maji na kusababisha mgawo uliokuwa unadumu kwa saa tano hadi nane na wakati mwingine maji yalikosekana kwa wiki nzima.

Aliongeza kuwa kazi inayoendelea kwa sasa ni maunganisho ya maji kwa wananchi kwenye maeneo mbalimbali.

"Nipende kuwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi kupata majisafi kwani DAWASA tuko kwenye program ya kuunganisha maji kwa mkopo," alisema.

Mradi wa Mlandizi - Chalinze - Mboga unahudumia wakazi zaidi ya 120,000 wa Chalinze na maeneo jirani.




# Wadau utalii wapewa somo afya, usalama mahali pa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa sekta ya utalii na hoteli mkoani Tanga wametakiwa kuzingatia viwango vya usalama na afya mahali pa kazi ikiwa ni mkakati wa kujiandaa kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi ukiwemo mradi mkubwa wa bomba la mafuta la Hoima-Tanga.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Sebastian Masanja, wakati akifungua kikao cha Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na wadau hao.

Masanja, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, alisema:

"Nitumie fursa hii kuwaeleza kwamba ninyi kama wadau wa sekta ya utalii na hoteli mna mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

"Sekta hii inashika nafasi ya pili baada ya sekta ya uzalishaji, hivyo pamoja na umuhimu huo nilioueleza, nawasihi kuzingatia taratibu muhimu za afya na usalama mahali pa kazi," alisema na kuongeza kuwa," alisema.

"Nadhani mmeshuhudia jitihada zinazofanywa na serikali ili kuinua sekta ya utalii iliyokuwa imeyumba kidogo kutokana na athari za janga la UVIKO-19. Jitahadi hizo zinaongozwa na Rais wetu mpendwa, Samia Suluhu Hassan ambaye aliweza hata kushiriki katika filamu ya The Royal Tour yenye lengo la kutangaza vivutio vyetu vya utalii.

"Lakini pia amekuwa akifanya jitahada nyingine nyingi za kuwavutia wawekezaji na hivyo kuzalisha fursa nyingi za kiuchumi ambazo endapo hatutaweza kufanya biashara zetu kwa kuzingatia sheria za nchi na viwango vya kimataifa ikiwemo masuala ya afya na usalama mahali pa kazi fursa hizi zitatupitia mbali," aliongeza.

Mkurugenzi wa OSHA, Alexander Ngata, ambaye alimwakilisha Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kikao hicho ni cha mashauriano na kuwataka washiriki kufuatilia kwa makini mada zilizoandaliwa pamoja na kueleza changamoto zinazowakumba katika utekelezaji wa masuala ya usalama na afya katika sehemu zao za kazi.

"Tumekuwa tukizungumza na baadhi ya wadau wa hapa Tanga lakini bado tunaona kama kuna vizingiti katika utekelezaji wa sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi hivyo tumeona ni vyema tukazungumza na wafanyabiashara wote wa Tanga ili kueleweshana na kutatua changamoto zilizopo.

Hii itawezesha biashara zenu kukua na kupata sifa za kushiriki katika fursa kubwa za kiuchumi ambazo miongoni mwa masharti yake muhimu ni kukidhi viwango mbalimbali yakiwemo masuala ya usalama na afya mahali pa kazi,"alisema Ngata.

Baadhi ya wadau walioshiriki kikao hicho wameeleza kuridhishwa na kikao hicho ambapo wameonesha matumaini makubwa kwamba maazimio yaliyowekwa yatatekelezwa.

Fatma Jokho, ambaye ni mshiriki wa kikao hicho alisema wanashukuru kikao kimeenda vizuri na kutoa maoni na kueleza changamoto mbalimbali pamoja na kupendekleza mambo mbalimbali katika kuboresha sekta hiyo.

Kikao hicho kilichofanyika kwa siku mbili kiliwahusisha wadau wa sekta za utalii na hoteli, usafirishaji, ujenzi, viwanda vidogovidogo na madini ambapo mada mbalimbali zimewasilishwa na kujadiliwa ikiwemo dhana nzima ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, Huduma za Ukaguzi mahali pa kazi pamoja na upimaji afya kwa wafanyakazi.




Mkuu wa Kitengo cha Maduka na Bidhaa za Intaneti cha Tigo, Mkumbo Myonga (kushoto) na Meneja Mkaazi wa Kampuni ya Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed, wakionyesha kwa waandishi wa habari simu janja za kisasa za Samsung S22, baada ya kuzindua, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mawakala EzyPesa wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu,** Pemba

WATOA huduma ya kifedha kwa njia ya mtandao wa Zantel, Ezypesa, kisiwani Pemba, wametakiwa kuhakikisha wanafuata sheria zote za utoaji wa huduma za fedha ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza na pia kuongeza ubora wa huduma hiyo kwa wateja.

Wito huo ulitolewa jana na Meneja wa Zantel, Bernadetha Israel, wakati alipokuwa akiwasilisha mada ya sheria za utakatishaji fedha na kuzuia uhalifu, kwa mawakala wanaotoa huduma za Ezypesa Kisiwani Pemba.

Alisema matatizo mengi yamekuwa yakijitokeza katika suala zima la utakatishaji wa fedha, ikiwa ni pamoja na kutumika kwa wizi na uhalifu.

"Siku hizi kuna SMS zinatumwa, tuma pesa kwenye namba hii, hao ni wahalifu na unapotumiwa lazima uwe makini nao na wewe unaweza kuituma Zantel tu," alisema.

Israel alisema ni vyema mteja akaonyesha utambulisho wake, ikiwamo kitambulisho cha mtanzania ikiwa ni mwenyeji wa nchi na si kudai huduma za kifedha na mhudumu akakubali moja kwa moja tu jambo ambalo linaweza kumuingiza katika matatizo.

Pia alisema ulimwengu hivi sasa unaenda kwenye digitali hivyo serikali malipo yake yote yanatakiwa kufanywa katika miamala ya kibenki au mitandao ya simu, lazima kufanya kazi kwa uaminifu mkubwa sana.

Akizungumzia kitengo cha mapato, meneja huyo alisema kuna mawakala wanafanya udanganyifu kwa kuwakata fedha wateja wao, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa kufuata sheria na ukweli.

Naye Ofisa wa EzyPesa, Eunice Alelyo, alisema lengo lao ni kuongeza minara, ili iweze kwenda vizuri, kwani mwaka huu wamekusudia kuboresha mambo mengi kwa lengo kutoa huduma bora kwa kuongeza huduma ya malipo ya serikali.

Alisema uwapo wa huduma bora unachangia kwa kiasi kikubwa chachu ya maendeleo nchini, huku akielezea faida mbali mbali zinazopatikana kupitia lipa kwa simu.

"Huduma ya lipa kwa simu ni moja ya huduma nzuri na rahisi sana, huduma inamfanya mfanyabiashara kutokutembea na pesa mkononi, imeweza kurahisisha mambo mengi kwa muda mfupi," alisema.

Naye Mkuu wa Huduma za Kifedha, Moses Alphonse, alisema lengo la mkutano huo ni kukumbushana kuhusu utaratibu na miongozo ya huduma za EzyPesa na huduma nyingine.

Kwa upande wao, mawakala wa huduma za EzyPesa, waliitaka kampuni ya Zantel kuangalia jinsi ya utoaji wa huduma zitakazo kidhi mahitaji ya watumiaji wa mtandao huo.

## ATE yazindua mafunzo kujengea wanawake uwezo katika uongozi

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimezindua mafunzo awamu ya nane ya 'Mwanamke na Uongozi' yakijumuisha zaidi ya wanawake 70 kutoka taasisi mbalimbali ili kuwawezesha kuingia kwenye bodi na kushiriki katika utoaji wa uamuzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba, aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa awamu hiyo ya mafunzo.

Alisema mradi huo ambao utachukua siku 14 darasani na miezi tisa ya kazi za vitendo, utawasaidia wanawake hao kutoka mashirika mbalimbali ya umma na ya kibinafsi kupata ujuzi muhimu wa uongozi ili kuwawezesha kufanya kazi vizuri katika mashirika yao.

Ndomba alisema kuwa mafunzo hayo yatatolewa kwa ushirikiano na Taasisi ya Uongozi ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI)

"Programu hii itakuwa ya manufaa na itawaunganisha wanawake kimkakati ili kuboresha utendaji wao, mafanikio ya kibinafsi na ya shirika na tunaamini hii itaongeza tija katika maeneo ya kazi," alisema. Ndomba aliongeza kuwa mradi huo pia unawahimiza wanawake kuwa viongozi wenye uwezo zaidi wa kushinda na kudhibiti hofu wakati wa kujadiliana katika masuala mbalimbali.

"ATE na ESAMI ziko tayari kuhakikisha zinatoa mafunzo kwa wanawake wengi zaidi kila mwaka na kuhakikisha kila mwanamke anapata kilicho bora zaidi kutoka katika programu hii. Kwa jumla, tuna Wanawake 73 waliojiunga nasi kwa kundi hili kutoka mashirika 34 ya sekta mbalimbali. Pia tuna wanawake kutoka mashirika ya serikali na mkuu wa wilaya na hii itaweka mazingira ya kujifunzia na kuwaendeleza viongozi waliojitokeza kwa ajili ya maendeleo ya biashara," alisema.

Ndomba alisema mafunzo hayo yanalenga zaidi kuongeza ushirikishwaji wa wanawake katika nafasi za uongozi katika ulimwengu wa ushirika, kuweka msingi wa maarifa kwa utendaji bora.

"Mwaka huu tunazindua programu mara baada ya kongamano letu la nne la mwaka la uongozi na mahafali ya kundi la saba," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ESAMI, Prof. Bonard Mwape, alisema wamekuwa wakishirikiana na ATE kuendesha mafunzo hayo tangu 2016.

Alisema kuwa utafiti mbalimbali umethibitisha kuwapo wanawake wengi katika nafasi za juu za uongozi, huongeza kasi ya maendeleo, hivyo kuwekeza kwao kunatakiwa kusisitizwa. Mafunzo hayo ambayo ESAMI inayafanya, alisema yatachukua nafasi yake katika kuondoa dhana potofu za kijinsia katika nafasi za juu kuwa wanawake hawana uwezo kitu ambacho si sahihi.



## Sera ya ajira kupitiwa upya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema matokeo ya utafiti wa hali ya nguvu kazi nchini umechangia kuanza mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na mkakati wa kuzalisha fursa za ajira nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Katika kuhakikisha tunaandaa sera, mikakati na programu za kukuza fursa za ajira ambazo zinaendana na hali halisi ya soko la ajira, serikali imefanya utafiti wa nne wa hali ya nguvukazi nchini na kutoa matokeo yake Novemba, 2021.

"Mara ya mwisho utafiti huu ulifanyika mwaka 2014 (takriban miaka saba iliyopita). Lengo la utafiti huu lilikuwa kupata viashiria muhimu vya soko la ajira vitakavyotumika katika kuhuisha, kufuatilia na kutathmini sera, mikakati na programu za soko la ajira," alisema Prof. Ndalichako.

Aidha, alisema matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa watu wenye uwezo wa kufanya kazi nchini ni milioni 25.9 (milioni 12.8 ni wanaume na milioni 13.1 ni wanawake) ambapo watu milioni 23.6 wana ajira sawa na asilimia 91.

Pia watu milioni 2.3 hawana ajira sawa na asilimia 9.0 (725,096 wanaume na 1,596,792 wanawake).

Aliongeza kuwa nguvukazi ya vijana ni watu milioni 14.2 sawa na asilimia 55 ya nguvu kazi yote na vijana wenye ajira ni milioni 12.5 sawa na asilimia 87.8.

Pia alisema sekta ya kilimo imeendelea kuongoza kwa kutoa ajira nyingi kwa vijana kwa kiwango cha asilimia 63.1 ikifuatiwa na sekta ya huduma asilimia 28.3 na sekta ya viwanda asilimia 8.6.

Vilevile, alisema serikali ya awamu ya sita imeendelea kuhakikisha mazingira ya kazi na haki za wafanyakazi nchini yanasimamiwa ipasavyo.

"Kwa kuimarisha taasisi za kazi nchini, kuboresha vyombo vya utoaji haki mahala pa kazi na kuwezesha upatikanaji wa haraka wa vibali vya kazi kwa raia wa kigeni,' alisema.

# RC Mtaka ageukia uwekezaji kilimo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameziagiza halmashauri za mkoa huo kuanzisha miradi ya mashamba makubwa yenye zaidi ya ekari 10,000 kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo.

Mtaka alitoa agizo hilo jana alipokuwa akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichofanyika jijini hapa.

Alisema mashamba hayo yatasaidia halmashauri kujiinua kiuchumi kupitia kodi zitakazolipwa kwa uwekezaji huo.

Mkuu huyo wa mkoa alitaka maeneo hayo yatakayotengwa yawe na miundombinu muhimu kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji watakaohitaji kulima mazao mbalimbali.

Aliitaja miundombinu hiyo kuwa ni barabara za kuingia kwenye maeneo hayo, maji na umeme ili kuwashawishi wawekezaji huku akitaka kila halmashauri ishirikiane na watoa huduma hizo ili kuhakikisha miundombinu hiyo inafika kwenye maeneo ya mradi husika kwa wakati.

Pia aliwataka kuhakikisha wanawasiliana na wataalamu wa afya ya udongo ili kuwashauri aina ya mazao yanayofaa kwenye eneo husika.

"Viongozi wa halmashauri mnatakiwa kuwasaidia wananchi katika kuhakikisha ardhi wanayomiliki inapimwa ili kuwa sehemu ya dhamana yao kwa taasisi za kifedha,"alisema.

Aliwaagiza kubadilishana uzoefu wa ubunifu wa miradi mingine ili kuinua uchumi wa Mkoa na wananchi wake.

Aidha, alisema kwa mwaka 2022/23 mkoa huo unatarajia kukusanya na kutumia Sh. bilioni 372 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 30.3 ya bajeti iliyopita ya mwaka 2021/22.

Ofisa Kilimo katika Sekretarieti ya Mkoa, Bernard Abraham, alisema ardhi ya Mkoa huo inafaa kwa kilimo cha alizeti.

Alisema Dodoma ni moja ya mikoa mitatu nchini ya kimkakati katika uzalishaji wa zao hilo na kwamba kuna mkakati wa kuhakikisha kila kaya inazalisha alizeti. Alisema kuna taasisi za kifedha zipo tayari kufanya kilimo cha mkataba kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) na watu binafsi katika kuhakikisha kilimo kinapata mafanikio katika Mkoa huo.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Janifa Omolo (kulia), akikagua ujenzi wa majengo ya hosteli ya wanafunzi wa chuo cha mipango yanayoendelea kujengwa katika eneo la Miyuji, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mkuu wa Chuo cha Mipango, Prof. Hozen Mayaya (wa pili kulia) na (wa tatu kulia) ni Mwenyekiti wa Baraza la uongozi wa chuo hicho, Prof. Martha Qorro. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Chuo cha Mipango chatakiwa kuongeza ubunifu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Jennifer Omolo, ameutaka uongozi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) kufanya kazi kwa ubunifu ili kuingia kwenye soko la ushindani.

Omolo aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na kamati ya uongozi ya chuo hicho sambamba na kukagua miradi ya ujenzi wa kampasi kuu ya Dodoma.

Alisema wataalamu wa chuo hicho wanatakiwa kuwa chachu ya mipango ya kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wananchi katika mipango wanayohitaji.

Naibu katibu mkuu huyo alisema chuo hicho ni kati ya vyuo ambavyo vinatazamiwa kwa kufanya mipango mizuri ya maendeleo kwa kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa, sambamba na kuwashirikisha wananchi mikakati ambayo wataifanya.

"Wataalamu lazima wajiulize kuwa wanaenda kubadilisha nini katika jamii. Kila tunachokipanga kiwe na manufaa kwa wananchi na kuwashirikisha pamoja na vipaumbele vyake," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Mipango, Prof. Hozen Mayaya, alisema IRDP imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 18.9 ikiwa ni asilimia 84 ya lengo la Sh. bilioni 22.5 kwa kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Februari, mwaka huu.

Prof. Mayaya alisema chuo hicho kimefanikiwa kulipa madeni na hadi kufikia Februari 28, mwaka huu, Sh. bilioni 2.6 zimelipwa kati ya deni la Sh. bilioni 3.1.

Alisema kati ya madeni yaliyolipwa madeni ya wafanyakazi ni Sh.bilioni 1.6 na madeni ya watoa huduma ni Sh. Milioni 995.3 ambapo hadi kufikia Machi mwaka huu chuo kinadaiwa Sh. milioni 426.9.

"Kati ya fedha hizi Sh. milioni 330.2 ni za wafanyakazi na Sh. milioni 96.8 ni kwa ajili ya watoa huduma. Chuo kimeweka mikakati wa kila mwezi kulipa deni hili kwa Sh. milioni 106.8 ili kuhakikisha linamalizika ifikapo Juni 30, mwaka huu," alisema.

Prof. Mayaya alisema kwa sasa chuo kinatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa kumbi tatu za mihadhara, ujenzi wa mabweni mawili, ujenzi wa mgahawa Kitumba Magu, ujenzi wa jengo la utawala Kitumba Magu na kununua ardhi kwa ajili ya upanuzi wa chuo. Katika miradi hiyo, alisema Sh. bilioni 10.9 zimetumika.

Alisema kati ya fedha hizo zilizotumika Sh. bilioni 7.7 ni ruzuku kutoka serikali kuu na Sh. bilioni 3.2 ni mapato ya ndani ya chuo.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo hicho, Prof. Martha Qorro, alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kusimamia chuo ili kuboresha mazingira kuwa rafiki kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia.





# Zanzibar na Uingereza nguvu moja mapambano ya mihadarati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar itaendelea kushirikiana na Uingereza katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya, uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Othman aliyasema hayo jana, ofisini kwake Migombani mjini Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi Mdogo wa Uingereza nchini, Rick Shearn.

Alisema serikali ya Uingereza imeahidi kuendelea kubeba dhima ya kuhakikisha kwa pamoja wanasimamia vyema masuala ya upatikanaji wa fedha za kusaidia masuala mbalimbali katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa Othman, Zanzibar inaendelea na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi na Uharibifu wa Mazingira na kwamba nchi hiyo imechukua juhudi za kuendelea kusaidia miradi ya kupambana na suala hilo.

Othman alisema hatua hiyo imetokana na ahadi ya nchi hiyo kukubali kuisaidia Zanzibar katika utekelezaji wa miradi ya kuijengea uwezo Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ikiwamo kusaidia nyenzo zitakazochangia kufanikisha mapambano hayo.

Akizungumzia Maendeleo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, Othman alisema hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na serikali ikiwa ni jitihada za kuifanya kutekeleza majukumu yake kwa maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar.

Naye Balozi Shearn alisema Uingereza inaridhika na utulivu na amani iliyopo Zanzibar iliyochangiwa na kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuahidi kuendelea kushirikiana sambamba na kuwataka wafanyabiashara wa nchi hiyo kuja kuwekeza Zanzibar.

Pia Balozi huyo alisema kwamba serikali yake itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maeneo mbalimbali likiwapo suala la mapambano dhidi ya dawa za kulevya na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira.



Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib (wa pili kulia), akipokea zawadi ya mkoba kutoka kwa Mwalimu, Siti Abdulazizi, uliotengenezwa na wanafunzi wa kituo cha elimu mbadala na watu wazima Rahaleo, mjini Zanzibar jana, alipowatembelea na kugawa zawadi kwa wanafunzi hao. Wa tatu kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakih. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Malipo kidijitali yanoga Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kupitia Wakala wa Serikali Mtandao 'eGovernment Zanzibar', zimetia saini makubaliano ya ushirikiano yatakayowezesha mifumo ya NMB kuingiliana na ile ya ZanMalipo.

Hatua hiyo itawezesha taasisi za SMZ kukusanya mapato kupitia matawi na mifumo ya kidijitali ya benki hiyo.

Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilifanyika jana mjini hapa huku NMB ikisema imejipanga kuimarisha ushirikiano huo ambao utakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi visiwani hapa na kwamba inaamini utakuwa wa karibu zaidi, endelevu na wenye manufaa kwa SMZ na taasisi zake.

Akizungumza kabla ya kutia saini makubaliano hayo ya mwaka mmoja yenye kipengele kinachoruhusu mazungumzo na kuyarefusha, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, aliipongeza SMZ chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa mageuzi chanya ya kiuchumi yanayochakatwa na kusimamiwa na serikali yake kwa ustawi wa taifa.

Zaipuna alibainisha kuwa makubaliano hayo ni chachu kwa taasisi yake kubuni suluhusho la Wazanzibari na taifa na kwamba maendeleo ya kidijitali kwa ulimwengu wa sasa hayaepukiki.

Alisema ushirikiano huo utakuwa na mchango chanya katika kuharakisha ukuzaji uchumi na kurahisisha utendaji wa serikali.

"Makubaliano haya ni kielelezo tosha kuwa serikali ya Zanzibar na NMB sasa tunaenda kushirikiana kuboresha huduma za ukusanyaji mapato na malipo, sambamba na kuwezesha mifumo yetu kuingiliana na ile ya ZanMalipo," alisema.

# Waziri awatoa hofu wananchi kuhusu ukosefu unga wa ngano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amewatoa hofu wananchi juu ya taarifa zinazosambaa katika mitandao ya kijamii kwamba unga wa ngano utakuwa adimu Zanzibar.

Amesema habari hizo si za kweli na kuwahakikishia kwamba bidhaa hiyo ipo ya kutosha zaidi ya mahitaji ya watu wa visiwani hapa.

Omar aliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja cha kujenga uhusiano na maelewano baina ya serikali na wafanyabishara wanaoingiza bidhaa nchini kilichofanyika katika ukumbi wa Shekh Idris Abdul Wakil, Kikwajuni.

Aliwaonya wanaosambaza taarifa hizo ambazo alisema ni potofu na zina lengo la kuweka taharuki kwa wananchi na kusababisha bidhaa hiyo ipande bei tofauti na bei iliyoruhusiwa.

Waziri alisema unga wa ngano upo na wazalishaji wanaendelea kuzalisha kutokana na ukweli kwamba bidhaa hiyo inazalishwa nchini.

"Wananchi wasisikilize taarifa hizi na kununua unga mwingi kuweka ndani kwani unga upo wa kutosha na kiwanda chetu kinazalisha mara mbili ya uzalishaji wa mwanzo," alisema.

Pia alisema pamoja na kupanda kwa bidhaa nje ya nchi, wafanyabishara hawatakiwi kuongeza bei za bidhaa bila kupata kibali na utaratibu wa kisheria .

"Elimu ya sheria ni ndogo sana kwa wafanyabiashara wetu na wanashindwa kufuata utaratibu huu lakini tayari tumeanza kukaa nao na tayari wapo waliokuja na kutuomba tufanye mapitio hayo," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaribu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema serikali ya Zanzibar itashirikiana na wafanyabiashara kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili ili kila mmoja kunufaika.

Alisema tayari wameunda timu maalum inayoshirikisha Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Maendeleo ya Biashara kukaa na watalaamu wa kodi wakiwamo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mkurugenzi Idara ya Biashara ili kujadili kwa pamoja changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi.

Waziri Hamza alibainisha kuwa serikali haitaki kuona wananchi wanapata tabu katika upataji wa bidhaa muhimu hasa kipindi cha kuelekea mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Alisema serikali inatambua kuwa kuna changamoto katika utumiaji wa mashine za kielektroniki (VFMS) hivyo ni jambo la msingi kuona ZRB inakaa pamoja katika kuangalia jambo hilo.

"Maazimio yetu si kupunguza kodi bali ni malalamiko waliyokuja nayo wafanyabiashara pengine tozo kwa kutumia mashine za kutolea risiti ndiyo inasababisha kuongezeka kwa bei. Kama itakuwa sababu ni lazima ZRB wakae na kuangalia hili ili isiendelee kuongezeka," alisema.

Mfanyabiashara kutoka Kampuni ya Yassir Provision Store, Walid Yakub Abdulkadir, alisema hivi sasa changamoto inayojitokeza ni kupanda wa bei za bidhaa duniani kote.

Alisema serikali inapoingiza bidhaa nchini imeweka bei elekezi kwa wafanyabiashara ili wananchi wasiumie lakini changamoto kubwa ni kutoa risiti za kielektroniki hasa kutoa risiti kwa bei waliyonunulia na si walioingizia nchini.



MAVOKO

UKURASA 12

JUMAMOSI MACHI 19, 2022

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# UZALENDO ZIRO Diamond awachefua wasanii

BAADHI ya wadau wa sanaa wameungana na mfalme wa muziki wa Taarab, Mzee Yusuph, ambaye ameonyesha kukasirishwa kwa kitendo cha Diamond Platnumz, kudharau tuzo za muziki zinazotolewa nchini.

Hivi karibuni, Mzee Yusuph, aliamua kumjibu mwanamuziki huyo ambaye alikaririwa akisema tuzo za muziki zinazotolewa kwake hazimfai, kuwa sawa na kuonyesha dharau.

Amesema haiwezekani yeye kama msanii aliyefanikiwa kusema maneno kama hayo aliyofananisha sawa na 'uchale' na si vizuri kucheza na sanaa ambayo yeye imemkuza.

"Unajua maneno mengine yanaumiza, mtu mmoja hawezi kucheza na sanaa yetu, kuna watu wengine nyuma wanakuja hivyo asiwakatishe tamaa haipendezi," amesema Mzee Yusuph.

Akimuunga mkono, Christopher Mwindaluka, amesema Diamond ana tatizo la kukosa watu wa kumshauri aseme nini na wakati gani kiasi ambacho anaweza kusema lolote bila kutafakari.

"Diamond kaanza muziki katika mazingira ya Kitanzania, anaposema yeye anashindana na watu wa nje pekee, haileti picha nzuri, ni lazima ajitafakari na uongozi wake uanze kumsaidia jinsi ya kuzungumza," amesema Mwindaluka.

Amesema kauli yake inaonyesha hana uzalendo wa kweli na nchi yake kama wanavyofanya wasanii wa Nigeria, ambao wanatangaza na kuthamini tuzo zinazotolewa nchini mwao.

"Hana uzalendo na nchi yake, wakati umefika kila mtu anayependa sanaa kulaani," ameongeza

Diamond alinukuliwa na vyombo vya habari akikataa kushiriki kwenye tuzo hizo kwa kile alichoeleza kukosa imani na jinsi zilivyoandaliwa.

"Kwangu YouTube naona inanitosha, lakini tuzo zinafaa kwa wasanii wengine nchini. Natazamia kupambana na watu wa nje na kuleta heshima Tanzania. Ukiniweka nashindana na msanii wa Tanzania ni kwenda kumkandamiza hatoniweza kwa sababu mimi nina vigezo vingi vya kufanya vizuri, kwanza nakipaji, na uwezo wa bajeti ya promotion, nacheza, mnyamwezi," amesema kwa kujigamba.

BASI SAWA

## Rich Mavoko unawapa watu presha



MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Rich Mavoko, amezidi kuwapa presha mashabiki wake kujua nini kipo ndani ya albamu yake mpya.

Rich Mavoko alipanga kutambulisha albam hiyo Machi 18 na kupeleka mbele hadi Machi 25 mwaka huu, kutokana na kupisha kumbukumbu ya Hayati John Pombe Magufuli.

"Album ya fundi itakufikia popote ulipo tarehe 25, mashabiki wasiwe na hofu watajua nini nimewaandalia," amesema.

## Ozzie 'Afungua moyo' akiwa Dodoma



Fungua moyo ni video mpya ya msanii wa muziki wa kizazi kipya, Happiness Ntalima, maarufu kama Ozzie kutoka makao makuu ya nchi jijini Dodoma.

Kipaji cha Ozzie hakijaanza katika singo hiyo mpya, ambayo ameitolea video, bali tayari ametamba na nyimbo zingine Teamo, Yahee na Yamoto.

"Namshukuru Mungu kwa kuweza kutoa video hii mpya na kutikisa Makao Makuu ya nchi naomba mashabiki wa kizazi kipya wanisapoti," alisema Ozzie.

Ozzie amesema singo hiyo ni safari ya kuandaa albamu yake ya kwanza ambayo bado hajaipa jina ingawa itakuwa ya video.

Video ya Fungua Moyo imetengenezwa na mwongozi Terry Leo wa Dodoma



## Jamila 'Afungua Njia' kumuimbia bwana

BAADA ya kung'ara kwenye nyimbo za kundi la Zabron Singers, mwimbaji wa muziki wa Injili Jamila Dotto, ameamua kutoka na wimbo wake binafsi.

Mwalimu na mtunzi wa nyimbo za kundi hilo, Japhet Zabron alidokeza ujio wa albamu ya mmoja ya waimbaji wake, hatimaye Jamila amekuwa wa kwanza kutambulisha wimbo wake unaoitwa Fungua Njia.

"Fungua Njia ndio wimbo wa kwanza ambao unamtambulisha Jamila Dotto kama mwimbaji binafsi akinishirikisha mimi, sasa unaweza kushiriki kwenye safari yake ya huduma," amesema Japhet Zabron.

# Mjomba Bure ya aghali

**Na Adam Fungamwango**

KUNA binadamu hapa duniani wanapenda sana utajiri kwa njia ya mkato. Yaani watapenda utajiri, lakini hawataki kuutolea jasho. Hao ni watu hatari kwa sababu wapo tayari kufanya kitu chochote ili mradi tu kutekeleza azma yake. Huyo yupo tayari kuutoa utu wake, kudharauliwa, kuchekwa, kunyanyaswa, na hata kutoa uhai wa mtu. Tena siyo mtu tu hivi hivi hata ndugu yake wa damu moja, wakati mwingine hata wazazi wake.

Filamu ya 'Mjomba' inaakisi hiki ninachokiandika hapa.

Inaanza kuonyesha maisha ya Sam na dada yake Davina. Waliishi maisha mazuri na mama yao ambaye alikuwa na uwezo mkubwa kiasi cha kuajiri wafanyakazi kwenye kampuni yake. Kifupi alikuwa tajiri.

Wanatembelewa na mjomba wao Suma ambaye anaongeza familia. Mama Sam anampeleka kaka yake kwenye kampuni yake akafanye kazi, lakini hataki kwa madai anafanyishwa kazi za udhalilishaji, ili hali yeye ni kaka wa tajiri mwenye kiwanda.


Dada yake anamwambia tatizo ni elimu yake ndogo, pia kutokuwa na ujuzi na uzoefu wa kitu chochote hapo.

Kuna siku ambayo familia nzima ilikwenda disco na kumuacha mama Sam nyumbani peke yake. Huku anavamiwa na majambazi na kuuawa. Kifo chake kinasikitisha watu wengi, na hakuna aliyekamatwa wala kushukiwa.

Siku isiyo na jina, Sam anamsikia mjomba wake Suma akiongea kwenye simu na watu walioonekana kuna pesa hajawamalizia, lakini maongezi yalionyesha kuwa walifanya kazi ya kumuua mama yake.

Hasira aliyonayo anakwenda kumwambia mjomba wake kuwa ndiye aliyesababisha mama yake afe.

Utajiri wa ghafla unamjia Suma kwa



sababu akawa kama ndiye mmiliki wa kampuni, badala ya Sam na dada yake Davina.

Suma alipoona Sam anaonekana kujua, akaagiza wauaji wake wale wakamuue Sam. Walipofika hawakumkuta yeye, bali dada yake Davina, wakamuua.

Hilo linamfanya Sam kutokuwa na la kufanya zaidi ya kulipiza kisasi. Akaanza kuua wote waliomuua mama yake na dada yake mmoja baada ya mwingine.

Suma, akaagiza wauaji wawili wa kukodi toka nje ya nchi. Hao ni Blade na Mr Karan. Wako fiti kweli kweli. Sam ambaye naye ni mjuzi wa sanaa wa mapigano, awali alipigwa. Lakini alikaa imara na kurejea tena na kuanza kupiga wote na kuwaua, mwisho makampuni na mali zote na nyumba zikarudi mikononi mwake.





## Mwijaku unamtafuta nini Diamond?

MSANII na mfuatiliaji wa mastaa nchini, Mwijaku, amesema tatizo la Diamond Platnumz, kutosikiliza ushauri linatokana na kuzungukwa na watu wasiojua.

Amesema hawezi kulumbana na Baba Levo ambaye amekuwa kama chawa wa mwanamuziki huyo na ndiye anayemfanya mwanamuziki huyo kufanya mambo yasiyopendeza.

Diamond amezungukwa na watu vilaza, watamshauri nini? Mimi ndiye nilimshauri atoe Albam, lakini kutokana na washauri wake akatoa EP ambayo kimsingi haina nyimbo nzuri," amesema Mwijaku.

## ZIMECHANUA NA KUNYAUKA KAMA MAUA

**Na Adam Fungamwango**

MWISHONI mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa mwaka 2000, kulizuka mapinduzi makubwa ya muziki wa dansi nchini na hasa ujio wa bendi za kotoka nchini Congo DR, kama Wenge Musica na Extra Musica, uliosababisha bendi nyingi zilizokuwa na muelekeo wa kuziiga nyimbo hizo kuundwa.

Baadhi zilikuwa ni za Wakongo wengi, Watanzania wakiwa wachache, lakini zingine Watanzania walikuwa wengi na wakongo wachache.

Hapo ndipo tulipoziona bendi zilizokuja kuwa maarufu kama Diamond Musica maarufu kama Wana Dar es Salaam Kibindankoi, FM Academia, African Stars 'Twanga Pepeta', TOT Plus Band, African Revolution 'Tamtama' na nyingine nyingi.

Hizi ni bendi zilizotingisha hasa nchi, zikiwa na wanamuziki wengi walioondokea kuwa maarufu kama Allan Mulumba Kashama, Adolf Mbinga, Ramadhani Masanja 'Banza Stone', Ali Choki, Mwinjuma Muumini na wengine wengi.

Waswahili wanasema kuwa kwenye msafara wa mamba na kenge wamo. Kwa bahati mbaya sana kipindi hicho hicho kuliundwa baadhi ya bendi zilizoondokea kuwa tishio kwa bendi maarufu kama Diamond Sound, Twanga Pepeta, lakini zikavuma kwa muda mfupi tu kabla hazijafa vifo vya ajabu.

Na zilipokuwa zikivunjika, baadhi ya wanamuziki wao vinara walikuwa wakichukuliwa na bendi hizo kubwa ambazo zenyewe kama Twanga Pepeta na FM Academia zipo hadi leo.

**Mchinga Sound**



Ni bendi iliyoanzishwa na mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, wakati huo akishika nyadhifa mbalimbali za Uwaziri serikalini. Ikumbukwe kuwa mheshimiwa huyo pia ni mtunzi mzuri hasa kwenye muziki wa taarab na muziki pia. Kwenye taarabu aliwatungia TOT wimbo wa "Kijeba', na kwenye bendi yake aliyoianzisha alitunga kibao cha 'Mti wa Mpingo'.

Ndiyo iliyowaibua kina Muumini. Ilipoanzishwa ilitishia ustawi wa bendi za Twanga Pepeta na Chumvi Chumvi ambayo baadaye ikageuka kuwa Tamtam, hata FM Academia.

Hata hivyo haikudumu, ikafa na kuwaachia mashabiki wengi wa muziki simanzi kutokana na vibao vyao vikali ilivyotoa.

**Stono Musica**

Bendi hii imetoka kwenye ubavu wa FM Academia. Baadhi ya wanamuziki wa bendi hiyo ambao wengi ni raia wa Congo walikamatwa kwa kuishi nchini bila kibali. Walipotoka walirejea FM Academia, lakini baada ya kutoa albamu moja tu ya 'Prisons' iliyotokea kuwa tishio, baadhi walijiengua na kwenda kuunda bendi ya Stono Musica chini ya Ndanda Kosovo wakajiita 'Wajelajela Original', yaani wao ndiyo hasa wale waliofungwa jela na si waliobaki FM Academia.

Iliishi kwa muda mfupi tu na kutoa vibao vikali kama 'Chini ya Ulinzi' 'Chocolate' na 'Binadamu'.

**Beta Musica**

Iliundwa na baadhi ya wanamuziki kutoka bendi mbalimbali zizokuwa na wanamuziki wengi wa Kikongomani kama FM Academia, Stono Musica, na Diamond Sound. Beta ilidumu kwa kipindi kifupi sana na wimbo wake maarufu sana ni 'Bana Beta'.

**Chuchu Sound**

Ni moja ya bendi matata sana, iliyosumbua bendi nyingi jijini Dar na Tanzania nzima. Yenyewe ilikuja na mageuzi makubwa, kwani pamoja na kupiga muziki wa aina ya bendi zingine, lakini ikaongeza na mduara ndani ikiwa na kina Jenico Flower, Omari Mkali, King Jiovani na wengineo.

Haijulikani ni nini kilisababisha bendi hii iliyopendwa mno ivunjike kwa muda mfupi tu, ikiwa ina vibao vikali kama 'Marafiki', 'Sitishiki', 'Hodi Hodi' na nyinginezo.

**Mokibo Sound**

Bendi hii ilianzishwa Mabibo jijini Dar es Salaam, nayo ni moja kati ya bendi zilizoanzishwa na kuleta ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi, lakini zikafa kifo cha ghafla na wanamuziki wake kusambaratika.



## Kim penzi limekupagawisha

WATU walioangalia kipindi cha Saturday Night Live, hawakuamini pale juu ya kifua cha Pete Davidson kumeandikwa jina la mpenzi wake Kim Kardashian.

Mchoro huo mpya wa tattoo wa rangi nyeusi una maneno makubwa ya "KIM", hivyo kuashiria mapenzi kati yao yapo motomoto.

Idadi kubwa ya watu walioangalia kipindi hicho wameamini mchoro huo umechorwa na Kim mwenyewe ili kuendelea kumuumiza mume wake wa zamani KanyeWest.



## Kylie huo ndio uzazi

MWANAMITINDO na mjasiriamali wa vipodozi kutoka Marekani, Kylie Jenner, amesema amepitia katika kipindi kigumu baada ya kujifungua mtoto wake wa pili.

Msanii huyo bilionea, amesema amefanyiwa uchunguzi kwa muda wa wiki sita mara baada ya kujifungua na kwamba hilo kwake sio jambo jepesi.

"Ni ngumu, nimepata uzoefu binafsi ilikuwa kama agizo kuliko kumpata binti yangu," amesema.

## Sarkodie ukikaa ndani utakula nini?

RAPA kutoka Ghana, Sarkodie, amesema upungufu wa mafuta unaosababishwa na vita kati ya Russia na Ukraine, utamfanya kuishi akiwa ndani ya nyumba yake.

Akizungumza na mashabiki wake kupitia mitandao ya kijamii, msanii huyo amewataka kuanza kuishi maisha hayo na hata wanapotaka kufanya mikutano watumie simu zao kukutana kupitia video.

"Kaeni ndani ya nyumba zenu na pale mnapotaka kukutana fungua Zoom mzungumze," amesema.





## Toke acha mkwara

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nigeria, Toke Makinwa, amewataka watu waweke heshima yake kwanza pale wanapolitaja jina lake.

Katika ujumbe wake wa Twitter, Makinwa, amesema jina lake limekuwa katika sekta nyingi nchini humo na kwamba imefikia wakati watu kujua thamani yake na sio kumuona kama mtu wa kawaida.

"Ngoja niwasaidie kidogo, mimi ni mtangazaji wa redio na runinga, ni mwendeshaji wa kipindi kikubwa cha African talk show, mwigizaji, mwandishi, mwanamitindo na mjasiriamali, hivo kuweni na heshima kabla hamjataja jina langu," ameandika.

## Maskini Kemi anawaliza wengi

MASHABIKI wa mwigizaji kutoka Nollywood, Kemi Afolabi, wamepatwa na mshtuko baada ya kusikia msanii huyo amebakiza miaka mitano pekee ya kuishi duniani.

Kulingana na Afolabi, daktari amemweleza ana miaka mitano ya kuishi kutokana na matatizo ya ugonjwa wa lupus.

"Kuwa na lupus huwezi kupata tiba, unahitaji tu kuchukua dawa kwa maisha yako yote," amesema Afolabi.



# Wanahabari wanavyotabasamu 'Mama' madarakani kwa mpya sita kuwabeba



Waandishi wa habari wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Romana Mallya**

LUGHA ya uswahilini ina msemo usemao "leo ndio leo". Hii inasadifu na hali halisi kwamba leo ni mwaka mmoja kamili wa Rais Samia Suluhu Hassan tangu alipoapishwa kushika uongozi wa taifa.

Si siri kila kundi lina 'jambo lake' katika tabasamu hilo la kuwa na 'mama' ofisini. Hapo ukigeuza sura uso kwa uso na wana ukoo wa wanahabari, nao wana jambo lao kwake.

Nipashe ilitaka kujua kipi kilichojificha nyuma ya pazia ya tabasamu la jambo lao. Haikuhitajika hata nguvu kubwa kupata majibu, maana mara moja wakaweka mezani orodha ya mambo sita yanayowapa bashasha.

Mafanikio hayo mzizi wake unaanzia kwenye ahadi ya Rais Samia, kisha yananyooshewa njia na swahiba wao mkongwe, Waziri Nape Nnauye, anayesimamia Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**WENYE FANI WAFUNGUKA**

Wanauzungumziaje mwaka mmoja wa Rais Samia, Mwenyekiti Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, anasema tangu aingie madarakani, Rais Samia amerejesha uhuru wa vyombo vya habari kwa kuyafungulia magazeti na TV mtandaoni zilizokuwa zimefungiwa.

"Ameelekeza kwamba sheria zipitiwe na kufanyiwa marekebisho ili ziendane na viwango vinavyokubalika kimataifa. Nia hii ninaiona ni ya msingi kwa sababu Rais amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha vyombo vya habari hata binafsi vinapewa matangazo na amekuwa akisema kwa uwazi.

"Yako mabadiliko makubwa na matarajio yetu ni makubwa kadri tunavyosonga mbele tunaamini atatenda makubwa zaidi," anasema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, anasema yako mabadiliko ya wazi yanayoonekana tangu Rais Samia alipoingia madarakani aliyaeleza waziwazi.

"Alitoa maagizo kuhusu vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe, bahati mbaya wakati huo watendaji walitoa tafsiri yao wakasema vinavyofunguliwa ni vyombo vya mtandaoni, magazeti hajayafungulia kitu ambacho hakikuwa sahihi, mama alivyosema ilikuwa wazi hakuna utata," anabainisha Kajubi.

Anasema katika kujihakikishia kuwa Rais Samia alikuwa anataka kuondokana na utamaduni wa kufungia vyombo vya habari, anarejea Februari 10, mwaka huu, Waziri Nape alipotangaza kuyafungulia magazeti ya MwanaHALISI, Mseto, Mawio na TanzaniaDaima na kuyapatia leseni wakati akizungumza katika kikao kazi na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari.

Jambo la pili, Kajubi anasema wakati wa awamu wa tano waliandikia barua Wizara ya Habari karibu mara tatu kuomba kukutana na waziri, lakini walifuatilia karibu miaka miwili jambo hilo bila mafanikio.

"Baada ya Rais Samia kuingia madarakani ndani ya miezi mitatu tumeweza kukutana na Waziri wa Habari wakati huo, Innocent Bashungwa, tulikutana na Waziri wa Katiba na Sheria, Palamagamba Kabudi. Hii inaonyesha serikali yake inaingilika.

"Kitu cha umuhimu kwa sababu Rais ameonyesha nia na mambo yameanza kubadilika ni wakati wa kubadili sheria, ili mambo haya yasitegemee roho nzuri ya mtu aliyeko madarakani.

"Ziwekwe sheria ambazo ni rafiki kwa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza, ili mtendaji yoyote atakayekuja awajibike kulingana na sheria, tusitegemee nia au roho ya mtu," anafafanua.

Kuhusu sheria zinazohitaji marekebisho, Kajubi anazitaja Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016; Sheria ya Makosa Mtandaoni ya mwaka 2015 na kanuni mbalimbali.

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, anasema ndani ya mwaka mmoja, wahariri wameona mafanikio makubwa katika tasnia ya habari.

"Kwanza vile vyombo vya habari ambavyo vilikuwa vimefungiwa, vikafunguliwa na kutakiwa vifuate sheria na taratibu zilizopo.

"Jambo la pili, ni matangazo. Kipindi cha nyuma matangazo mengi yalikuwa yakienda kwenye vyombo vya habari vya serikali ikilinganishwa na vyombo binafsi, kwa upande huu wa matangazo vyombo binafsi pia tunasherehekea," anasema.

Beatrice anasema katika uteuzi mbalimbali aliofanya, Rais Samia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, wameshuhudia waandishi wa habari wakiteuliwa katika nafasi mbalimbali na huko waliko wanafanya vizuri.

"Tunatumaini ataendelea kuteua waandishi wa habari wengine ili kumsaidia. Pia, katika safu ya uongozi wake tumeshuhudia wanawake waking'ara katika nafasi mbalimbali zikiwamo sekta nyeti, ndani ya mwaka mmoja tumeshuhudia unafuu wa uhuru wa vyombo vya habari.

"Ombi langu kwa Rais Samia asituchoke pindi anapokuwa na muda tunaomba aweze kukutana na wahariri na waandishi wa habari tunaamini kukutana huko mara kwa mara yapo atakayoyapata kutoka kwetu na sisi kutoka kwake.

"Hata hili la kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa lilitokana na nafasi aliyotoa kwetu ya kukutana naye," anabainisha.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA Tan), Salome Kitomari, anasema kwa kipindi cha mwaka mmoja wameshuhudia mabadiliko ya demokrasia, hususani kwenye vyombo vya habari.

"Kwa sasa vyombo vya habari vinaweza kufanya majukumu yake hususani kukosoa, wajibu wa vyombo vya habari ni kuelimisha, kuburudisha na kukosoa. Kukosoa ndiyo huleta matatizo kwa watawala.

"Sheria, kanuni ambazo zilikuwa na matatizo ambazo wadau tulikuwa tukizipigia kelele muda mrefu, Waziri wa Habari ametuita wadau kujadiliana, juzi Waziri ameeleza zipo kanuni ambazo zimefanyiwa marekebisho.

Salome, anatoa mfano wa kanuni inayoruhusu mtu kurusha matangazo mubashara mitandaoni, ambayo awali ilikuwa mpaka waombe kibali.

"Maana yake ni nini? Jamii ilikuwa ikikosa taarifa kwa sababu tu urasimu wa mfumo uliokuwapo. Kanuni ya kusajili ilikuwa Sh. 100,000 imepunguzwa hadi shilingi 50,000, kuwa na TV za mtandaoni ilikuwa ni Sh. milioni moja imepungua hadi shilingi 500,000, : anaeleza Salome na kufafanua:

"Hii ni ahueni kwa sababu sekta ya habari inakua na teknolojia nayo inakua, kama sekta hii inakua maana yake wapo vijana wataanzisha TV za mtandaoni na kujiajiri."

Mkuu huyo wa Misa Tan, anafafanua kuwa mazingira ya aina hiyo yanasaidia kuendelea kujenga imani na kumwondolea mtu kuwaza mtawala anawaza nini.

"Uhuru wa uhariri una afadhali. Vyombo vya habari haviingiliwi sana vinaandika ilimradi vinajikita kwenye misingi ya kisheria na tamaduni za nchi.

"Upo utayari wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusiana na Sheria ya Huduma ya Habari ambayo kimsingi ina mambo mengi ambayo yanakwaza vyombo vya habari."

Anasema uhuru wa kupata habari, nao una vifungu vinavyowakwaza, wakati katika uhalisia serikali inafanya mambo mengi ambayo Watanzania wanapaswa kuyajua.

"MISA Tan tunaridhika kwa kiasi kikubwa na hatua ambazo serikali inachukua za kuikuza sekta ya habari, sekta ya habari ni huduma lakini hapo hapo ni biashara imeajiri watu.

"Tumeshuhudia vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa vimefunguliwa, yale magazeti hayawanufaishi tu wamiliki wapo walioajiriwa humo na wanachangia uchumi wa nchi kwa kulipa kodi," anahitimisha.

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Vituko vya makonda, utingo wa zamani

## •Kupiga bodi ya gari, kumhamasisha dereva •Kuning'inia mlangoni •Kwa nini ziliitwa daladala?

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja nikiwa ndani ya daladala, alitokea mzee mmoja akawa anamwambia konda maneno yafuatayo.

"Makonda na utingo wa siku hizi mna raha sana, mnakaa ndani, mnafunga mlango, mnachukua nauli kwa raha sana, abiria akitaka kuteremka, mnamfungulia mlango, halafu mnafunga du!"

Konda akamuuliza yule mzee kama yeye alikuwa konda wa daladala zamani, na kwa nini walikuwa hawafungi milango?

Mzee akamjibu maneno haya "Ndiyo, mimi nilikuwa konda, na siyo kama daladala za zamani zilikuwa hazifungi milango, ilikuwa hakuna kabisa, ilikuwepo kama tundu tu, ni kama nyumba iliyowekwa flemu ya mlango, lakini mlango wenyewe haupo, watu wanaingia na kutoka tu."

Mazungumzo hayo yalinifanya nikumbuke mbali sana. Katika miaka ya mwanzoni mwa miaka ya 1980. Waliokaa jijini Dar es Salaam kipindi hicho ambao kwa sasa watakuwa wametapakaa sehemu mbalimbali duniani, watakumbuka jinsi daladala za zamani zilivyokuwa zikisomba watu.

Kabla hatujaenda mbali sana, tuangalie majina ya baadhi ya daladala enzi hizo ambazo ndiyo zilikuwa zinaanza kufanya kazi ya kusafirisha abiria.




**MAJINA YA DALADALA**

Njia ya Kariakoo, Posta, Temeke na Tandika kulikuwa na daladala kama Riziki kwa Mungu, Tim Yulee, Golo, Kainkwa, Kita Ngoma, Dunia Muzima, na Ubungo Posta na Kariakoo kulikuwa na Matema Beach, Shella Beach, Ole wao Wafuatao nyayo za Simba, Scholastika, Mshua, Dau la Mnyonge, na nyinginezo.

Mwananyamala, Kariakoo, Posta na Stesheni kulikuwa na daladala maarufu zaidi wakati huo, Simba Luwala, Chako Changu, Again, Najimunisa, na mengineyo, Mwenge Kariakoo na Posta kulikuwa na Makadidi, Kiabakari, Jadide, Pugu Kariakoo, Buguruni, Vingunguti, Posta, kulikuwa na Sea Never Dry, Masumin, Jaribu Tena, Inter Programmes na nyinginezo.

**MUASISI WA DALADALA**

Huwezi kuzitaja daladala hizi zote bila kumtaja aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania wakati huo, Edward Moringe Sokoine.

Yeye ndiye aliyeagiza magari binafsi yaanze kusafirisha abiria, baada ya Shirika la Usafiri (UDA) kuzidiwa uwezo na kusababisha shida kubwa ya usafiri jijini Dar es Salaam. Abiria walikaa vituoni hata masaa matatu mpaka manne, bila UDA kuonekana. Na hata likija hiyo vurugu ya kugombania kupanda, inakuwa si ya kawaida.

Sokoine alikuwa waziri mkuu katika vipindi viwili tofauti.

Kwanza ilikuwa kuanzia Februari 13, 1977 hadi Novemba 7, 1980 alipojiuzulu mwenyewe baada ya afya yake kuzorota kufuatia pilikapilika wakati wa vita vya Idd Amin.

Februari 23, 1983, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alimteua tena kuwa waziri mkuu, baada ya afya yake kuimarika.

Aliporudi tena ofisini, akakuta hali ya usafiri Dar es Salaam ni mbaya sana.

UDA, lilikuwa limeelemewa na abiria kiasi kwamba halikuweza tena kumudu biashara hiyo ya kusafirisha abiria peke yake.

Lakini sheria ya nchi wakati huo haikuruhusu watu binafsi kusafirisha abiria jijini Dar es Salaam, badala yake mikoani tu.

Ndipo kama waziri mkuu, akawaita wafanyabiashara wenye kuweza kununua mabasi ili watoe huduma ya usafiri. Na si wafanyabiashara tu, bali hata Makampuni na Mashirika ya Umma nayo yakaambiwa yatoe huduma hiyo. Ndipo tulipoanza kuona hata mabasi ya wafanyakazi ya Mashirika na Makampuni na Taasisi mbalimbali za Kiserikali, yakianza kutoa huduma, au kufanya biashara ya kusafirisha abiria, baada ya kupeleka wafanyakazi maofisini na pia kabla ya kuwarudisha majumbani.

**MAANA YA DALADALA**

Wakati huo UDA ilikuwa inatoza nauli kiasi cha shilingi tatu. Lakini magari binafsi yalipoitikia wito wa Sokoine, yalianza kutoza kiasi cha shilingi tano.

Kipindi hicho kulikuwa na sarafu moja ya shilingi tano, iliyokuwa na matuta matuta kama tairi la trekta, ikiitwa 'gwala.' Kama vile haitoshi, wakati huo shilingi tano ya kitanzania ilikuwa na thamani ya dola moja ya Kimarekani. Kwa hiyo ile pesa ya 'gwala' ikaanza kuitwa 'dala', wakiwa na maana dola.

Makonda na utingo wa wakati huo wakawa wanaitia abiria, "Kariakoo nauli dala, Posta nauli dala, Stesheni nauli dala, Shule ya Uhuru nauli dala." Wakiwa na maana nauli ni shilingi tano, na hiyo walikuwa wanataka kutofautisha nauli zao na zile za UDA ambazo ni shilingi tatu.

Kuanzia hapo abiria, na Watanzania wote wakaanza kuyaita magari hayo kwa jina la 'daladala', kutokana na kuchukua abiria kwa nauli ya dala, ambayo ni shilingi tano wakati huo.

**VITUKO VYAO**

Kutokana na kutokuwa na utaratibu, wala sheria yoyote kama ilivyo sasa, nadhani kutokana na kwamba biashara hiyo kwa watu binafsi ndiyo ilikuwa inaanza, mabasi yalikuwa yanajaza sana kupita kiasi.

Abiria walikuwa wananing'inia, miili yao ikiwa nje kabisa, lakini mikono yake tu, ndiyo ilikuwa imepata sehemu fulani ya kushikilia. Picha ya makala hii, inaeleza hali halisi iliyokuwepo wakati huo. Na hata askari wa usalama barabarani walikuwa hawawakamati. Ilionekana kama ni jambo la kawaida tu.

Konda au utingo wakati huo ilikuwa ni lazima ujue kudandia basi, na kuwahi kushuka wakati gari linatembea, ili kupisha abiria wateremke.

Makonda na utingo ilikuwa ni nadra sana kuwakuta wapo ndani ya gari, badala yake wao walikuwa wananing'inia mlangoni kama nyani, sambamba na abiria wengine waliokuwa na uwezo wa kufanya hivyo, au kupenda kufanya hivyo. Pamoja na kwamba ni kweli kulikuwa na shida kubwa ya usafiri na magari yalijaza sana, lakini baadhi ya abiria hawakupenda kusubiri mengine, ndiyo waliokuwa wakijikuta akining'inia.

Yoyote ambaye hakuweza kuning'inia, au kudandia wakati tayari abiria wameshajazana mlangoni na gari linaondoka, au kuteremka wakati gari halijasimama vizuri, hakuweza kufanya kazi ya ukonda au utingo.

Pia walikuwa na tabia ya kushinikiza madereva kuendesha magari kwa kasi au kulifukuza daladala lingine na kulipita kwa kupiga miluzi, akiashiria kukubaliana na mwendo mkali, au kumtaka aongeze na maneno mengi kama "kamua kamua baba asituache huyo".

Walikuwa na tabia pia kuwaashiria tayari abiria wameshapanda na sasa dereva anatakiwa kuondoka kwa kupiga bodi la gari kwa nguvu, na sauti kali ya kushtusha inatokea, na hata wakati dereva anatakiwa kusimama kwenye kituo, ishara ni bodi litapigwa kwa mkono au mguu atajua mwenyewe. Na hata wakati mwingine gari iko kwenye mwendo mkali, unaweza kushtukia bodi linapigwa kwa nguvu, akiashiria kumpongeza dereva na kumtaka aendelee na kazi nzuri, wakati huo yeye amening'inia mlangoni na abiria wengine wenye uwezo wa kuning'inia. Hii ndiyo iliyosababisha msamiati wa 'kupiga debe' au 'wapiga debe', ingawa baadaye ikabadilika kidogo ukaja kwa wale wanaoitia abiria vituoni. Na hata wanaoning'inia wakaitwa 'utingo' kwa sababu wanatinga kwa kuning'inia mlangoni, sehemu kubwa ya miili yao ikiwa nje ya basi. Ni sahihi kabisa kuwa daladala za zamani hazikuwa na milango ya kufunga.

Kwa sasa kila kitu kimebadilika, daladala zina milango, abiria akitaka kupanda au kushuka inafunguliwa na baada ya hapo inafungwa. Wanakaa ndani ya basi, hawaning'inii tena. Hawapandishi abiria mpaka wakang'ang'ania nje. Sheria zimewekwa vizuri kwa sasa. Ila majina na misamiati kama daladala, utingo, kupigadebe imebaki kama ilivyo.

**KIFO CHA SOKOINE**

Sokoine alifariki Aprili 12 kwa ajali ya gari akitokea Bungeni Dodoma na gari lake aina ya Benzi.

Aprili 12, 1984 wakati akitoka Dodoma bungeni, Benzi lake liligongwa na Toyota Land Cruiser eneo la Dakawa, Morogoro.

Mwili wake ukaletwa Dar es Salaam kisha ukapelekwa uwanja wa ndege kwa ajili ya kusafirishwa kwenda Monduli Arusha kwa mazishi.

Wamiliki wa daladala walitoa usafiri bure siku hiyo Dar es Salaam nzima kwa watu waliotaka kwenda uwanja wa ndege kuusindikiza mwili wa kiongozi huyo, kumuenzi mtu aliyewapa dili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yafedheheshwa vita vya Ukraine, yadaiwa kupoteza wanajeshi 14,200



Wanajeshi wa Russia wakiwa mstari wa mbele wa vita ndani ya vifaru vyao wakiusogelea mji mkuu wa Kyiv. **PICHA GETTY IMAGES**

**KYIV,** UKRAINE

WANAJESHI 14,200 wa Russia wameuawa tangu kuanza kwa vita ambayo imechukua siku 24 hadi leo.

Wizara ya Ulinzi ya Ukraine, ilisema katika taarifa yake ya kila siku kwenye Facebook, kwamba idadi hiyo ya wanajeshi waliouawa ni tangu mzozo huo uanze.

Kupata idadi kamili ya majeruhi kwa kila upande kumeonekana kuwa changamoto, huku Russia na Ukraine zikidai idadi ni ndogo.

Katika taarifa yake ya Machi 3, Russia ilidai kuwa wanajeshi wake 498 waliuawa katika mapigano, lakini imekaa kimya juu ya kuachiwa kwa takwimu zaidi tangu wakati huo.

Wakati huo huo, maofisa wa Marekani, walisema Alhamisi idadi ya waliojeruhiwa wa Russia inaweza kuwa zaidi ya 7,000, hadi 14,000.

### DUTERTE ASEMA NCHI YAKE HAITATUMA WANAJESHI IKIWA.....

Rais wa Ufilipino Rodrigo Duterte, alisema hatapeleka wanajeshi wake kupigana nchini Ukraine iwapo Marekani itahusika katika mzozo huo.

Marekani na Ufilipino zina mkataba wa ulinzi wa pande zote mbili ambao unaahidi mataifa yote mawili kusaidiana ikiwa nchi yoyote ingeshambuliwa na mtu wa nje.

"Sitafanya hivyo ikiwa Wamarekani watashiriki vita na wako hapa, kwa nini nitume wanajeshi wangu? Sio vita vyetu vya kupigana,"alisema Duterte katika hotuba yake siku ya Alhamisi.

"Ikiwa vurugu zitaenea na vita kwa namna fulani vifike hapa, hiyo itakuwa ngumu sana. Alimradi mimi ndio Rais, sitamtuma hata mwanajeshi wangu mmoja kwenda vitani," aliongeza.

Baada ya kuingia madarakani katikati ya mwaka 2016, Duterte amechukua hatua za kuimarisha uhusiano na Russia, huku akikosoa sera za usalama wa Marekani.

Duterte amekutana na Rais wa Russia, Vladimir Putin mara mbili mjini Moscow.

Katika hotuba yake alimtaja Putin kama rafiki wa kibinafsi na siku za nyuma aliripotiwa kumwita kiongozi huyo kama "sanamu" lake.

Hata hivyo, alilinganisha mzozo wa Ukraine na vita vyake dhidi ya madawa ya kulevya, ambayo imeshuhudia maelfu ya washukiwa wakiuawa wakati wa operesheni za polisi tangu kuanza mwaka wa 2016.

"Putin anaua raia huko, niliua tu wahalifu kwa sababu ya dawa za kulevya." Alisema

### UKRAINE IMEIFEDHEHESHA RUSSIA

Imeelezwa Ukraine inazidi kuidhalilisha Russia katika uwanja wa vita, anasema mtaalam wa kijeshi kutoka Uingereza.

Prof. Michael Clarke, Mkurugenzi wa zamani wa Taasisi ya Huduma ya Kifalme ya Muungano (RUSI) alisema Warussia wanafanya kila makosa ya vitani ambayo yanawezekana kufanyika.

Akiongea kwenye kipindi cha jana cha Radio 4 cha BBC, alieleza "Wao wanaonekana kama vikosi ambavyo havikuwa tayari kabisa, ambavyo havikuwa vimefikiria jinsi kampeni kuu inavyoweza kuwa". alisema

"Waukraine wanazuia hatua za Russia katika maeneo yote na hata wanaendesha mashambulizi ya kukabiliana kwa sasa yenye ufanisi. Warussia wanapoteza vifaa na wanajeshi wengi."aliongeza

Prof Clarke alisema Ukraine ina mfumo wa amri na udhibiti wa uwanja wa vita kama wa Nato uliojengwa kwa usaidizi kutoka nchi za Nato tangu 2014.

Shambulio la kiwanda cha kutengeneza ndege huko Lviv asubuhi ya jana linaweka wazi Warussia wanaenda kutafuta miundombinu ambayo inaweka ndege za Kiukreni angani", alisisitiza.

Kushambulia mji wa magharibi kilomita 70 kutoka mpaka wa Poland pia ni jaribio la kuzitia hofu nchi za Magharibi kutokana na kuwasaidia Waukraine.

Afrika yatakiwa kuchagua upande

Takriban watu milioni tatu wamekimbia makazi yao kutokana na vita hivyo, kulingana na Umoja wa Mataifa.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, alisema mataifa ya Afrika hayawezi kubaki kutounga mkono upande wowote katika vita vya Ukraine.

Akizungumza na BBC, Linda Thomas-Greenfield, alibainisha kuwa katika kura iliyopigwa kwenye mkutano wa Baraza Kuu wiki mbili zilizopita kuonesha kuchukia uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine, nchi 17 za Afrika zilijizuia na nyingine nane hazikupiga kura kabisa.

Balozi huyo alisema hakuwezi kuwa na msingi kwenye kutoegemea upande wowote, na kwamba mgogoro huu haukuwa mashindano ya Vita Baridi kati ya nchi za Magharibi na Russia.

Thomas-Greenfield, alisema Marekani ilikuwa ikisaidia kutafuta vyanzo mbadala vya bidhaa ambazo nchi huagiza kutoka Russia.

Mwanadiplomasia huyo pia alisema nchi yake itaunga mkono pendekezo la Afrika Kusini la kupatanisha Russia na Ukraine.

### CHINA YAKUTANA NA BALOZI WA RUSSIA

Ofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Cheng Guoping, alikutana na balozi wa Russia nchini humo juzi ili kubadilishana mawazo kuhusu uhusiano wa nchi hizo mbili.

Kulingana na chombo cha habari cha Reuters, kikinukuu taarifa ya wizara hiyo kuwa kamishna wa Mambo ya Nje na Masuala ya Usalama katika wizara hiyo alikutana na Andrey Denisov wa Russia kwa lengo la kubadilishana mawazo kuhusu ushirikiano wa pande hizo mbili dhidi ya ugaidi na usalama.

Mkutano huo unakuja huku kukiwa na hofu kwamba China itakubali ombi la Russia kutoa msaada wa kijeshi katika uvamizi wake nchini Ukraine.

Marekani ilionya kuwa haitasita kuitoza gharama kubwa China ikiwa itaisaidia Russia moja kwa moja na zana za kijeshi.

### BILIONI 1 KUZUIA UHABA WA CHAKULA AFRIKA

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), inapanga kuchangisha dola bilioni moja katika muda wa wiki moja kusaidia uzalishaji wa kilimo barani Afrika kutokana na uhaba wa chakula unaotokana na vita inayoendelea nchini Ukraine.

Nchi nyingi za Kiafrika zinaitegemea Russia na Ukraine kwa usambazaji wa nafaka.

Somalia, Benin, Misri na Sudan zinaongoza kwenye orodha ya nchi ambazo zinategemea nchi hizo kwa zaidi ya asilimia 70 ya ngano zinazoagiza kutoka mataifa hayo mawili.

"AfDB inaona ongezeko hili la bei ya ngano, mahindi na maharagwe ya soya kama uwezekano wa kuzidisha uhaba wa chakula na kuongeza mfumuko wa bei," Rais wa AfDB Akinwumi Adesina alisema.

Alisema ataitisha mkutano wa mawaziri wa fedha na kilimo barani Afrika ili kutekeleza mpango huo.

Kupitia mfuko huo, AfDB inalenga kuongeza uzalishaji wa mpunga, ngano, mahindi na soya kwa kutumia teknolojia zinazostahimili hali ya hewa, zikiwemo aina za mazao zinazostahimili joto na ukame.

Aina ya ngano inayostahimili joto tayari imejaribiwa nchini Sudan na Ethiopia.

Kulingana na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Biashara na Maendeleo (UNCTAD), takriban mataifa 25 ya Afrika yanaagiza zaidi ya theluthi moja ya ngano yao kutoka Russia na Ukraine.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 248 YA MWAKA 2021**
**BAINA YA**
**KALANTINI STANLEY MTAMBALA……………..MDAI**
**DHIDIY YA**
**PAULO MTORO………………..MDAIWA**
**KWA: PAULO MTORO – POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 22.03.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:-** Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

**Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya Mwezi Februari, 2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na: MMC/LD/15339**
**Tarehe: 11.03.2022**
**MUSTAPHA RAMADHANI,**
**S.L.P 217, MOROGORO.**
**YAH: NIA YA KUTOHUISHA MILIKI YA KIWANJA NA. 128 KITALU"B" MSAMVU**

**Rejea kichwa cha habari hapo juu.**

Kiwanja Na.128 Kitalu B Msamvu hapo awali kilitolewa kwa ndugu Mustafa Ramadhani kupitia Hati Na. 35881 iliyotolewa muda wa miaka 33 kuanzia tarehe01/01/1988 kwa matumizi ya makazi miliki hiyo ilikwisha muda wake tangu tarehe 30/12/2021.Aidha mwaka 1998 ilitolewa pia Barua toleo (Ofa) kwa Ndugu Macmillan S. Moshy ambaye ameendeleza kwa kujenga nyumba ya makazi.
Kupitia fungu la 32 la sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 Ofisi haina nia ya kuendelea kuhuisha milki ya Ndg Mustafa Ramadhani kwani alishindwa kuendeleza kiwanja hicho kwa kufuata kanuni na taratibu.
Aidha tunakusudia kumilikisha milki hii kwa Ndg Macmillan S.Moshy ambaye mpaka sasa ndiye ameendeleza kiwanja hicho.
Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro S.L.P 587 Morogoro ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya barua hii.

VALENCY H.K
K.N.Y MKURUGENZI WA MANISPAA, MOROGORO

**VALENCY H.K**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya …...TANGA**
**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi….. SHAURI DOGO Na…6/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: KALIMUDDIN YUSUFALI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: SHEHREBANU MOIZ YUSUFALI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11/4/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo 18/03/2022**

---

ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T.LTD & COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULOPEWA NA SHIRIKA LA HUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SIDO) TUTAFANYA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 26/03/2022 KUANZIA SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA KIWANJA KIMOJA CHENYE UKUBWA WA 632.4 SQ/M KIPO IYUMBU MTAA WA MULINYI KARIBU NA SHULE YA MSINGI IYUMBU, MALI YA VIOLET FELIX MUTASA MDAIWA WA SIDO.

**KWA MAWASILIANAO TUPIGIE NO. 0713913150**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha Kinguluira**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi……1..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ABDUL IDD WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA IDDI ABDUL NGAJA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21/03 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 08/03/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LAMADAI NAMBARI 15/2022**
**MDAI: ELIAS MATHAYO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA ANNA JUMA**
**WA**
**TANZANIA BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 23/03/2022 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo 09 tarehe 03 Mwezi 2022

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE GEITA.

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SEBASTIAN J.ODODA** anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 861 BJR,** injini namba **D1103AEDU** na chassis namba **MD2A18A21GWB73429.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/25896/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0754834181 au 0739834181.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

SALMA IDDI SELEMANI anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye NAMBA ZA USAJILI MC 991 BNZ, INJINI NAMBA PFZWGJ37510 na CHASSIS NAMBAMD2A21BZ27GWJ9 2485. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAAARIFA: DAR/KIJ/RB/58598/2022

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

# NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-18

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Jan kwa asilimia kubwa alikuwa anaongea ukweli, lakini mengine alipindisha kidogo.

Ukweli ni kwamba mpango mzima wa kuweka makaratasi kwenye mkoba ambao uliwekwa chini ya daraja mara mbili, ulikuwa ni wa kwake na hakumjulisha mjomba Ken.

Walichokubaliana na Ken ni kuweka kwenye mkoba shilingi milioni 15 ambazo zilipatikana kutoka kwa Challa.

Ambacho Ken hakukijua, ni kwamba Jan alizichukua pesa hizo na kwenda kuziweka nyumbani kwake, na kujaza makatarasi matupu.

Kikubwa ni kwamba Jan hakutaka watekaji wale wachukue mkoba na kumuacha Diana bila kukamatwa. Na ndiyo maana awali alikwenda kumtaarifu Afande Marco, na mara ya pili aliwapigia maafande wa kituo cha Polisi Magomeni waje kwenye tukio.

Alijua kama wangeuchukua mkoba na kwenda kukuta hakuna pesa, basi hiyo peke yake ingekuwa tiketi ya kifo cha Diana. Kama wakikamatwa hata kama mkoba utakuwa na makaratasi haitakuwa na hatari yoyote. Na kama alivyotarajia ndivyo ilivyokuwa.

"Kwa nini ulipoweka mkoba haukuondoka na badala yake ukaamua na wewe kujiweka kwenye hatari, wakati tayari ulikuwa umeshatuambia twende kwenye eneo la hatari? Huoni kama ulikuwa unahatarisha maisha yako?" Afande alizidi kummiminia maswali Jan.

"Afande mimi ni raia. Raia pia ana wajibu wa kuisaidia polisi kusaka wahalifu, na ndiyo maana umeona nimekuwa moja kati ya msaada mkubwa kwenye hili. Mimi ndiye niliyepeleka mkoba wa mwanzo, ambao ulikuwa na makaratasi kwenye daraja la Mfugale, lakini siku hiyo hawakuja kwa sababu walipata taarifa za kiitelejensia kuwa askari wamejua kila kitu.

Baada ya kutuambia sasa tubadilishe na kutuambia sasa pesa tuzipeleke kwenye daraja la Magomeni Kajima, mimi ndiye niliyepeleka tena, lakini sikuondoka, nikajisweka kwenye vichaka vilivyopo pembeni mwa daraja, kwenye mto Msimbazi. Kabla ya hapo niliwapigia simu polisi, na mimi mwenyewe nilitaka kupambana. Nilifanya hivyo kwa ajili ya mpenzi wangu Diana, Mfano kama ningekaa nyumbani nigejuaje kama watamuachia au la wakipata pesa zao." Jan alifunguka.




**Ambacho mkuu alichokuwa hajui ni kwamba Jan, anafahamu fika uhusiano wa Diana na Afande Marco, lakini aliahidiwa na mwanamke huyo asiwe na wasiwasi, ipo siku mambo yatakaa sawa.**

"Afande Marco ulikuwa unamfahamu?" Aliuliza Mkuu wa Kituo.

"Ndiyo namfahamu."

"Unamfahamu vipi?"

"Nilitambulishwa na Diana kuwa alimsaidia siku moja alipopata ajali ya bodaboda." Alijibu.

Mkuu wa Kituo aliuliza swali hilo kimtego. Lakini hakutaka kwenda mbali zaidi. Marehemu Afande Marco alikwishamwambia kuwa msichana aliyetekwa ni mpenzi wake. Lao anashangaa kusikia pia kijana yule Jan ni mpenzi wake pia.

"Inawezekana, kuna baadhi ya wanawake bwana, anaweza kuwachanganya wanaume hata watatu, mkawa mnafahamiana, lakini hamjui kama mnachangia mwanamke mmoja." Alijiambia mwenyewe.

Ambacho mkuu alichokuwa hajui ni kwamba Jan, anafahamu fika uhusiano wa Diana na Afande Marco, lakini aliahidiwa na mwanamke huyo asiwe na wasiwasi, ipo siku mambo yatakaa sawa.

Mkuu huyo hakuwa na la zaidi kwa Jan, alimruhusu kuondoka pamoja na Diana.

Kwa mara ya kwanza baada ya miezi miwili, Jan na Diana walionana tena.

Walikumbatiana, na mabusu tele tele. Mkuu wa kituo kama kuna kitu alitaka kusema, lakini hakufanya hivyo.

Aliwaacha. Nao wakatoka nje kuelekea maeneo ya Magomeni Usalama kwenye kituo cha Taxi

"Tupeleke Mwananyamala." Jan alimwambia dereva. Ilichukua dakika 30 hivi kufika huko.

Waliingia ndani. Mwanzo ni kama walikuwa wanaangalia, lakini kila mmoja alikuwa na hamu na mwenzake.

Kila mmoja alikuwa na mengi ya kumwambia mwenzake.

"Kweli ni wewe Diana kweli?" Aliuliza Jan wakiwa sasa wapo peke yao chumbani.

"Ni mimi mpenzi wangu."

"Siamini, uko hai kweli?"

"Niko hai mpenzi."

"Mungu mkubwa, sikutarajia kukuona tena uko hai kwa jinsi hali ilivyokuwa."

"Ni kweli, kutekwa ni kitu kibaya sana, ukweli hata mimi nilikuwa sipati usingizi. Siyo kwa sababu ya kutekwa, bali kukuwaza wewe. Nilikuwa najua unaumia sana kunikosa, lakini mimi nilikuwa silali kwa kukuwaza mpenzi wangu." Diana alipomaliza kusema hivyo aliangua kilio cha kwikwi, huku akimkumbatia kwa nguvu Jan.

Jan alitulia. Alijua Diana analia machozi ya furaha yaliyochanganyikana na uchungu. Uchungu ni kwa sababu ya kutekwa. Hakupata muda wa kulia, kutokana na kuhofia usalama na uhai wake. Moyo wake ukaweka sugu, hivyo alishindwa kulia hadi pale atakaposhuhudia mustakabali wa yote. Machozi ya furaja kwa sababu ameponyeka kutoka kwenye mdomo wa mamba. Alikuwa karibu na kifo zaidi kuliko uhai.

Kwa namna ya ajabu ambayo hakutarajia, si tu kwamba ameokolewa, lakini yupo sehemu salama zaidi. Sehemu anayoipenda kuliko vyote. Yupo na mtu aliyetokea kumpenda. Yupo mikononi mwake. Anahisi joto lake. Hayo yote yakichanganyika, ndipo anapolia machozi ya uchungu iliyochanganyika na furaha.

"Hakuna chochote kibaya kilichokupata tangu umekwenda huko?" Ni swali ambalo alitegemea, lakini hakulitegemea kwa wakati ule.

"Najua, najua una wasiwasi na wale manyang'au kuwa labda wangeweza kunifanyia chochote. Ingewezekana kama wao ndiyo wangekuwa vinara wa kundi lile.

Usichokijua ambacho hata askari nimewapa siri kuwa kinaongozwa na wanawake watatu. Wao wanawatumia wanaume kuwakamata wanawake. Ni wanawake matajiri, lakini kazi yao ndiyo hii. Wanajua ukimkamata mwanamke, inakuwa ni rahisi sana ndugu, mume, mpenzi kutafuta pesa haraka ya kumkomboa. Wakiwateka wanawake wanapeleka kwao,

kwa hiyo wanakuwa salama. Hawawafanyi chochote. Ila unazabuliwa vibao viwili vitatu siku ambayo unashikishwa simu ili kuongee na ndugu zako, kuonekana kuwa kuna mateso sana.

Wanachohitaji ni pesa tu, lakini huduma zote chakula, matibabu unapata. Ni watu wazuri, hasa wale wanawake ambao huwezi kuona sura zao kamili." Diana alitiririka na kumpoza Jan ambaye kiasi fulani wivu ulikuwa umeshaanza kumuingia.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# MAONO, MKALEKWA ULINGONI KUSAKA CHAMPION WA KITAA

**Na Saada Akida**

FAINALI ya kusaka bingwa wa ngumi wa shindano la Champion wa Kitaa itafanyika kesho kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mratibu wa fainali hizo, Bakari Khatibu alisema maandalizi yamekamilika na mabondia watakaoshiriki watapima uzito leo tayari kwa ajili ya kumpata mshindi wa taji hilo.

Khatibu alisema fainali hiyo itakuwa na mapambano 15 ambayo yatachezwa kwa uzito tofauti na itashirikisha mabondia 20 waliofika hatua hiyo.

"Mapambano matano yatakuwa yanasindikiza fainali hizo huku pambano kuu litakuwa kati ya bondia, Maono Ally dhidi ya Salehe Mkalekwa," alisema mratibu huyo.

Aliongeza kutokana na maandalizi yaliyofanyika, wanatarajia kuwa na fainali zenye ushindani kwa sababu mabondia wamejiandaa vyema kuonyesha vipaji vyao ili kuwavutia mapromota mbalimbali.

"Tumefanya makubaliano rasmi na mabondia ambapo wamejiandaa vizuri, wamejifua kwa kufuata programu rasmi na hiyo imelenga kusapoti fainali hizo," alisema Khatibu.

Aliwataja mabondia ambao watapambana kwa ajili ya kuwania ubingwa wa Champion wa Kitaa ni Shabani Kimimbi dhidi Abdallah Muhumba, Hamad Mkude atazichapa na Said Mkola huku Uwesu Mbetu atachuana na Muhidin Kavunga.

Mambondia wengine watakaopambana ni Swahibu Ramadhani dhidi ya Said Uwezo, Hussein Mkalekwa dhidi ya Jadi Salehe, Maski Mushi dhidi ya Hassan Kube, Peter Toshi dhidi ya Oswarld Maneno, Hussein Saidi dhidi ya Ally Lubanja, Viguru Shafii dhidi ya Hemed Rashid na Omary Mpemba atazichapa dhidi ya Mohammed Manyindi.

Watakaosindikiza fainali hizo ni pamoja na Hassan Ndoga dhidi ya Adam Mbega, Ally Ngwando dhidi ya James Kibazangwe, Abdallah Pazi (Dulla Mbabe) dhidi ya Amour Sheikh na Mussa Said dhidi ya Selemani Galile.




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: YANGA SC.**

# Riadha Singida kusaidia afya

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

CHAMA cha Kijamii cha Golden Brothers kwa kushirikiana na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), kimeandaa mbio za barabarani zitakazofanyika Julai 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya LITI mkoani hapa.

Mbio hizo zimepata baraka kutoka katika Baraza la Michezo la Taifa (BMT), zinatarajiwa kushirikisha wanariadha 2,500 ambao watakimbia umbali wa kilomita tano, kilomita 10 na half marathoni (kilomita 21).

Mwenyekiti wa Golden Brothers, Raymond Msangi alisema lengo la kuandaa mbio hizo ni kutaka kuchangia mahitaji ya kuboresha huduma za afya hasa kwa upande wa mama na mtoto.

Msangi alisema kwa mara ya kwanza chama chake kimeandaa mbio hizo kufuatia utafiti uliofanyika baada ya kutembelea Hospitali ya Rufaa ya Mandewa na kubaini wodi ya wazazi na watoto zinahitaji kuboreshwa na kupatiwa vifaa vya matibabu.

"Fedha zitakazopatikana katika mbio hizo zitatumika kusaidia jamii, hususani katika kuboresha afya ya mama na mtoto," alisema Msangi.

Aliongeza pia wanalenga kuibua vipaji vipya vya wanariadha na kutoa fursa ya kuitangaza Singida kupitia mbio hizo ambazo zitahusisha washiriki kutoka mikoa yote ya Tanzania pamoja na nchi za jirani.

Alitaja kauli mbiu katika mbio hizo ni Kimbia Uache Alama na kuwataja wadhamini waliothibitisha kusaidia ni viongozi wa siasa, viongozi wa dini, kampuni za simu, wafanyabishara na wadau mbalimbali wa michezo mkoani Singida.

## SPUTANZA yaipa tano TFF 2022/23

**Na Adam Fungamwango**

CHAMA cha Wachezaji wa Soka Tanzania (SPUTANZA), kimelipongeza Shirikisho la mchezo huo nchini (TFF), kwa kuweka kanuni ya kuzibana timu kulipa madeni ya nyuma ya wachezaji kabla ya kupata leseni ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2022/23.

Mwenyekiti wa SPUTANZA, Mussa Kisoki alisema kanuni hiyo itawasaidia wachezaji wenye madai kulipwa kwa wakati huku wale wenye madeni ya muda mrefu pia kupata stahiki zao.

Kisoki alisema kwa muda mrefu walikuwa wakililia kanuni hiyo iwekwe ili iwe mwarobaini wa malalamiko ya wachezaji ambao wamekuwa wakizitumikia timu kwa muda mrefu lakini kulipwa ilikuwa mtihani.

"Nawapongeza sana TFF kwa kuliona hili, wamesikia kilio chetu. Ni jambo la kuhuzunisha na kusikitisha mchezaji anaiacha familia yake, anakwenda kukaa kambini kwa muda mrefu na kuitumikia timu kwa nguvu na jasho lake, lakini baadhi wamekuwa wakimaliza mikataba huku bado wanadai," alisema Kisoki.

Jumanne iliyopita, TFF pamoja na kuzitaka klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Championship na Ligi Daraja la Kwanza kwenda kuchukua fomu kwa ajili ya msimu wa 2022/23, ilitoa angalizo haitatoa leseni kwa timu ambayo itakuwa inadaiwa na mchezaji mpaka pale itakapomaliza kulipwa deni hilo.

## African Sports yaipania JKT TZ

**Na Cheji Bakari, TANGA**

LICHA ya kuwa katika nafasi ya chini kwenye msimamo, uongozi wa African Sports ya jijini Tanga umesema bado wana matumaini ya kufanya vyema katika Ligi ya Championship inayoendelea.

African Sports inajiandaa kuifuata JKT Tanzania katika mechi ya Ligi ya Championship itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Isamuhyo ulioko Bunju, Dar es Salaam.

Katibu wa African Sports, Hatibu Enzi alisema timu yake inaendelea vyema na mazoezi na anaamini watapata matokeo chanya kwa kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo.

Enzi alisema licha ya kuwa katika nafasi ya 12 katika msimamo wa ligi hiyo, bado wana nafasi ya 'kupindua meza' katika mechi zilizobakia.

"Sisi tunacheza ligi hatuangilii tupo nafasi ya ngapi, ila sasa hivi tunajiandaa na mchezo wetu dhidi ya JKT Tanzania utakaochezwa Bunju Dar es Salaam, tumedhamiria kuondoka na pointi tatu muhimu," Enzi alisema.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD ANUKIA BARCA

BARCELONA wameonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24. Mwaka 2019 Rashford alisaini mkataba wa United wa kulipwa pauni 200,000 kwa wiki unaoishia Juni, mwakani lakini amekua na kiwango kibovu msimu huu. (***Manchester Evening News***)

### RONALDO KUBAKI UNITED

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 anajiandaa kusalia klabuni hapo msimu ujao, huku kocha wa muda, Ralf Rangnick akitarajiwa kuondoka. (***AS***)

### HAZARD KUTUA ARSENAL

ARSENAL wanataka kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Chelsea aliyeko Real Madrid, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31. Mbelgiji huyo alijiunga Real Madrid mwaka 2019. (FootMercato)

### NUNEZ APANDA DAU

KLABU ya Benfica imetangaza thamani ya mshambuliaji wake raia wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, ni pauni milioni 67, Nyota huyo aliisaidia klabu hiyo ya Ureno kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nunez anazivutia pia klabu za Arsenal, Manchester United na Newcastle. (***Mirror***)

### GRAVENBERCH SOKONI

KINDA wa miaka 19 wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ryan Gravenberch anasakwa na Manchester United. (***The Athletic***)

### RICE KUIKACHA CHELSEA

WACHEZAJI wanaowaniwa na Chelsea kuna wasiwasi wasiweze kujiunga na mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, anaonya wakala. Klabu hiyo imekua ikihusishwa na wachezaji kadhaa akiwamo kiungo wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23. (***Daily Mail***)

### JORGINHO KUBAKI CHELSEA

WAKALA wa Jorginho amesema kipaumbele kikubwa kwa sasa cha mchezaji huyo mwenye miaka 30 ni kusaini mkataba mpya wa kubakia Chelsea, licha ya kusakwa na magwiji wa Serie A, Juventus. (***90Min***)

### CONTE BADO YUPO

ANTONIO Conte hataondoka Tottenham msimu huu, amesema mlinda mlango na nahodha Mfaransa Hugo Lloris. Gwiji huyo anaamini Mtaliano huyo sio wale "wanaokata tamaa mapema katika mazingira yoyote". (***Evening Standard***)

### ORIGI KUTUA MILAN

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 26, anajiandaa kujiunga na AC Milan mwishoni mwa msimu huu. (***Fabrizio Romano***)

### GOMEZ ANUKIA FULHAM

KLABU ya Fulham inawataka walinzi wa Liverpool, Joe Gomez na Neco Williams. Mchezaji wa kimataifa wa England, Gomez mwenye umri wa miaka 24 anauzwa na wekundu hao kwa bei ya pauni milioni 23. Mlinzi wa pembeni wa Wales, Williams mwenye miaka 20, kwa sasa anacheza kwa mkopo Craven Cottage. (***Express***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AINGIWA HOFU KUHUSU EL CLASICO

### ●●● Kocha huyo asema mchezo huo utakuwa mgumu kwake na kuongeza kesho itakuwa...

**ISTANBUL,** UTUTUKI

HUKU akisifu ushindi wa timu yake dhidi ya Galatasaray katika michuano ya Ligi ya Europa, Kocha wa Barcelona, Xavi amesema haiwezi kuwa na maana yoyote akifikiria mechi ya El Clasico itakayochezwa kesho.

Blaugrana hao watalazimika kurejea haraka kutoka katika ushindi wa jumla wa mabao 2-1 wa Alhamisi, na kutinga robo fainali katika michuano ya Ligi ya Europa, huku safari ya kuelekea Santiago Bernabeu dhidi ya Real Madrid ikisubiriwa.

**"Leo (juzi) ulikuwa mchezo muhimu, kwa sababu tunachezea Kombe la Europa," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.**

"Tunataka kufika mbali katika mashindano haya, na tuna furaha kubwa kuwa katika robo fainali, kwani tunastahili kuwepo.

"Ndiyo, tuko katika hali nzuri kwa sasa kuelekea El Clasico, lakini hiyo haimaanishi chochote.

"Nimepitia kila kitu kuhusu michezo hiyo, nikicheza vibaya na kisha kushinda au kucheza vizuri halafu wakatufunga. Jumapili itakuwa hadithi tofauti, ngumu sana na ngumu."

Ushindi wa Barcelona mjini Istanbul uligubikwa na majeraha kwa Sergino Dest na Gerard Pique, ambao wote walilazimika kutoka kipindi cha pili.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,042

MECHI KALI
ASTON VILLA
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.83
X | 3.37
2 | 2.44

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# SANCHO, RASHFORD WATEMWA ENGLAND

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford na winga, Jadon Sancho wameachwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ambacho kitacheza michezo ya kirafiki dhidi ya Uswisi na Ivory Coast kwenye dimba la Wembley, imefahamika.

Rashford hajaitwa katika kikosi cha England tangu kumalizika kwa fainali ya Euro 2020 ambapo alikuwa miongoni mwa wachezaji waliokosa penalti, huku siku za karibuni akiwa kwenye kiwango kibovu na katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano iliyopita ilisambaa video ikimwonyesha akiwatolea maneno machafu mashabiki.

England imeshafuzu katika mashindano ya Kombe la Dunia nchini Qatar, na wanataka kuitumia hii michezo ya kirafiki kama maandalizi na kuweka umoja kwenye kikosi chao.

Harry Maguire na Luke Shaw ni wachezaji pekee kutoka Manchester United walioitwa na Kocha, Gareth Southgate.

Kikosi kamili; Magolikipa: Jordan Pickford (Everton), Nick Pope (Burnley), Aaron Ramsdale (Arsenal).

Walinzi: Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Conor Coady (Wolves), Marc Guehi (Crystal Palace), Reece James (Chelsea), Harry Maguire (Manchester United), Tyrone Mings (Aston Villa), Luke Shaw (Manchester United), John Stones (Manchester City) na Ben White (Arsenal).

# Benzema apewa nafasi kujitetea

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Karim Benzema, atapewa nafasi ya pili ya kuthibitisha kutokuwa na hatia katika kesi ya ulaghai ya Mathieu Valbuena, baada ya adhabu kusimamishwa hapo awali.

Kesi hiyo ilizua utata ikimhusu mchezaji mwenzake wa zamani wa Ufaransa, Valbuena, ambaye alidaiwa kukashifiwa baada ya mkanda wa ngono kuangukia kwenye mikono ya matapeli.

Benzema amekuwa na msimamo wa kutokuwa na hatia tangu alipokamatwa kwa kesi hiyo, lakini Novemba, mwaka jana alipewa adhabu



ya faini ya Euro 75,000 na adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja iliyositishwa.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon alipatikana na hatia hiyo, ingawa alikwepa kukaa gerezani.

Benzema ameendelea na majaribio yake ya kusafisha jina lake kama ilivyoripotiwa na ESPN kupitia Caught Offside, mahakama za Ufaransa zimempa rufaa ambayo itasikilizwa msimu huu wa joto.

Nyota huyo alifukuzwa kwenye Timu ya Taifa ya Ufaransa kwa miaka saba kati ya 2014 na 2021, kabla ya kurejea chini ya Didier Deschamps kwenye michuano ya Euro 2021.

## HABARI MICHEZO


# 2,431,860

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/03/22 | 18:00 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.51 | 3.29 | 2.65 |
| 02. 19/03/22 | 18:00 | Reading vs Blackburn | 2.60 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 19/03/22 | 18:15 | Eupen vs Mechelen | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 04. 19/03/22 | 20:45 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.48 | 3.45 | 2.70 |
| 05. 19/03/22 | 23:00 | Nantes vs Lille | 2.87 | 2.97 | 2.63 |
| 06. 20/03/22 | 14:30 | Venezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 20/03/22 | 15:30 | Jahn Regensburg vs Paderborn | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 08. 20/03/22 | 16:00 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 09. 20/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Montpellier | 2.40 | 3.45 | 2.80 |
| 10. 20/03/22 | 17:00 | Empoli vs Verona | 3.20 | 3.40 | 2.20 |
| 11. 20/03/22 | 18:00 | Ponferradina vs Eibar | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 12. 20/03/22 | 18:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.41 | 3.34 | 2.89 |
| 13. 20/03/22 | 20:00 | Roma vs Lazio | 2.34 | 3.41 | 2.96 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 19/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 3671 | Aston Villa vs Arsenal | 2.83 | 3.37 | 2.44 |
| 18:00 | 3525 | Ballymena Utd vs Glentoran Belfast | 4.05 | 3.61 | 1.74 |
| 18:00 | 3541 | Reading vs Blackburn | 3.04 | 3.14 | 2.31 |
| 18:00 | 3667 | Celtic vs Ross County | 1.14 | 7.52 | 15.83 |
| 18:00 | 3727 | Hearts vs Livingston | 1.67 | 3.69 | 4.83 |
| 18:00 | 3902 | Alloa Athletic vs Peterhead | 2.21 | 3.42 | 2.94 |
| 18:00 | 3931 | Glenavon vs Cliftonville Belfast | 3.27 | 3.56 | 1.95 |
| 18:00 | 3971 | St Johnstone vs Motherwell | 2.42 | 3.00 | 3.05 |
| 18:00 | 4114 | St Mirren vs Dundee Utd | 2.23 | 3.05 | 3.34 |
| 18:00 | 4156 | Raith Rovers vs Inverness | 2.43 | 3.18 | 2.78 |
| 18:00 | 4262 | Crusaders Belfast vs Warrenpoint | 1.16 | 6.37 | 12.55 |
| 18:00 | 4274 | Rotherham vs Shrewsbury | 1.58 | 3.89 | 5.32 |
| 18:00 | 4430 | Stoke City vs Millwall | 2.29 | 3.08 | 3.13 |
| 18:00 | 5006 | Albion Rovers vs Forfar Athletic | 3.42 | 3.42 | 1.94 |
| 18:00 | 5117 | Portadown FC vs Coleraine FC | 4.82 | 3.96 | 1.56 |
| 18:00 | 5171 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 18:00 | 5238 | Hull City vs Luton Town | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 18:00 | 5245 | Hammarby vs Elfsborg | 2.24 | 3.43 | 2.76 |
| 18:00 | 5766 | Linfield Belfast vs Dungannon Swifts | 1.13 | 7.14 | 13.51 |
| 18:15 | 1587 | Kfum Oslo vs Viking | 5.01 | 3.85 | 1.56 |
| 18:15 | 2395 | Eupen vs Mechelen | 2.86 | 3.45 | 2.30 |
| 18:15 | 5820 | Elche vs Valencia | 2.66 | 3.17 | 2.71 |
| 18:30 | 1234 | Tondela vs FC Arouca | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 18:30 | 2628 | VVV Venlo vs Emmen | 3.99 | 3.51 | 1.82 |
| 19:05 | 5684 | Hajduk Split vs Lokomotiva Zagreb | 1.46 | 4.13 | 5.77 |
| 19:30 | 3390 | Maribor vs NK Celje | 1.65 | 3.81 | 4.34 |
| 19:30 | 4494 | Lechia Gdansk vs Gornik Leczna | 1.52 | 3.84 | 5.56 |
| 20:00 | 1854 | Lanus vs Banfield | 2.50 | 3.12 | 2.64 |
| 20:00 | 5507 | Inter vs Fiorentina | 1.51 | 4.49 | 5.78 |
| 20:00 | 5574 | Pafos FC vs Anorthosis Famagusta | 2.73 | 3.17 | 2.58 |
| 20:00 | 5719 | FC Cincinnati vs Inter Miami CF | 2.13 | 3.55 | 3.25 |
| 20:00 | 5748 | St. Gallen vs FC Luzern | 1.86 | 3.65 | 3.80 |
| 20:00 | 5935 | New York City vs Philadelphia Union | 1.69 | 3.85 | 4.80 |
| 20:15 | 2941 | Middlesbrough vs Chelsea | 5.92 | 4.25 | 1.49 |
| 20:30 | 2141 | Osasuna vs Levante | 1.88 | 3.45 | 4.20 |
| 20:30 | 4024 | Bayern Munchen vs Union Berlin | 1.17 | 7.54 | 12.89 |
| 20:45 | 4926 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.07 | 3.48 | 3.23 |
| 21:00 | 3169 | Santa Clara vs Belenenses | 1.58 | 3.69 | 5.91 |
| 22:00 | 2773 | Sandnes Ulf vs Stromsgodset | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 22:00 | 2846 | Twente vs PEC Zwolle | 1.67 | 3.66 | 4.79 |
| 22:00 | 3242 | Lech Poznan vs Jagiellonia | 1.30 | 4.82 | 8.09 |
| 22:30 | 1767 | LA Galaxy vs Orlando City | 1.76 | 3.85 | 4.30 |
| 22:30 | 3603 | Arka Gdynia vs GKS Katowice | 1.72 | 3.62 | 4.15 |
| 22:30 | 4583 | BSC Young Boys vs FC Zurich | 1.77 | 3.83 | 4.03 |
| 22:45 | 4865 | Cagliari vs AC Milan | 5.38 | 3.99 | 1.60 |
| 23:00 | 2815 | Atlanta United FC vs Montreal Impact | 1.71 | 3.94 | 4.49 |
| 23:00 | 3253 | NEC Nijmegen vs Sparta Rotterdam | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 23:00 | 3330 | Rayo Vallecano vs Atletico Madrid | 3.80 | 3.25 | 2.05 |
| 23:00 | 4649 | Nantes vs Lille | 2.89 | 2.94 | 2.64 |
| 23:30 | 3524 | Vitoria Guimaraes vs Sporting Lisbon | 4.83 | 3.74 | 1.66 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MWALALA KURITHI MIKOBA YA MEDO COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Bernard Mwalala anatajwa huenda akatangazwa kuwa Kocha Mkuu mpya wa Coastal Union ya jijini Tanga ambayo iliachana na aliyekuwa kocha wake, Melis Medo.

Mwalala ambaye haitokuwa mara yake ya kwanza kuifundisha timu hiyo, kwa sasa anaifundisha Kakamega Homeboyz ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Kenya, anatajwa ndiye aliyependekezwa na jopo ya ufundi likiongozwa na Juma Mgunda, ingawa imekuwa ngumu kwa viongozi kuweka wazi.

Hivi karibuni, uongozi wa Coastal Union ulitangaza kupokea wasifu kutoka kwa makocha mbalimbali wakiomba kuinoa timu hiyo, akiwamo kocha wa zamani wa Simba, Goran Copunovic, ambaye huyo waliweka wazi hakuingia kwenye tano bora.

Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi alisema wako kwenye hatua za mwisho za kumpata Kocha Mkuu na kuwataka mashabiki wao kuwa na utulivu.

"Kwa sasa hatuwezi kusema ni nani tunatarajia kumtangaza, zinabaki kama tetesi, lakini tutamtangaza kocha wetu hivi karibuni," alisema Wandi.

Hata hivyo, vyombo vya habari vya Kenya, ikiwamo mitandao ya kijamii imeonyesha wasiwasi kama Mwalala anaweza kuondoka kwenye klabu hiyo, kwa sababu amekuwa na matokeo mazuri.

Kakamega Homeboyz inaongoza Ligi Kuu Kenya ikiwa na pointi 49 baada ya kucheza mechi 23, ikiizidi pointi nane Tusker FC iliyoko katika nafasi ya pili, hivyo Mwalala ana nafasi kubwa kuweka rekodi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ambao utamfanya kupandisha thamani yake.

Mwalala aliwahi kuifundisha Coastal Union mwaka 2012, lakini alikuwa straika hatari alipokuwa katika kikosi cha Yanga mwanzoni mwa miaka ya 2000.



Wachezaji wa Ihefu SC wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Kengold itakayochezwa Machi 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya. **PICHA: MTANDAO**

# Polisi Tanzania, TRA kujipima

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuazimisha mwaka mmoja wa Rais, Samia Suluhu Hassan madarakani, Polisi Tanzania inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa wa mkoa wa Kilimanjaro, TRA FC utakaofanyika kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, aliliambia gazeti hili lengo la mechi hiyo ni kumpongeza na kuunga mkono uongozi wa Mama Samia.

"Kesho (leo) tutakuwa na mchezo wa kirafiki wenye lengo la kuungana na rais wetu kuadhimisha mwaka wake mmoja akiwa madarakani," alisema Mketo.

Kocha huyo alisema wachezaji wao wanaendelea vizuri na mazoezi na kuongeza wanashukuru hawana majeruhi ndani ya kikosi chao.

Aliongeza mchezo huo pia utawasaidia katika maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Aprili Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ushirika.

# Michezo

Jumamosi Machi 19, 2022
Nipashe

UKURASA 22




Benzema apewa nafasi kujitetea




Winga wa Simba, Pape Ousmane Sakho (kushoto), akisalimiana na shabiki wa timu hiyo (hayuko pichani), aliyekwenda kuwapokea kwenye Uwanja wa Ndege mjini Cotonou, Benin baada ya kuwafuata wapinzani wao Asec Mimosas kwa ajili ya mechi ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho nchini humo. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba: Tutawashangaza

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi kikitua salama katika jiji la Cotonou nchini Benin jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema watacheza kwa tahadhari mechi dhidi ya Asec Mimosas kutoka Ivory Coast ili wakamilishe malengo ya kusonga mbele katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika mapema.

Pablo alisema wamejipanga kuchukua tahadhari kubwa kwa sababu inaonekana katika michuano hiyo kila timu inakuwa na nguvu kubwa inapocheza kwenye uwanja wa nyumbani.

Kocha huyo alisema wamejiandaa vyema ingawa baadhi ya wachezaji wanakabiliwa na uchovu wa kucheza mechi nyingi mfululizo, lakini hilo halitawazuia kuhakikisha wanapata ushindi dhidi ya Asec Mimosas ambayo pia kiuhalisia itakuwa inacheza ugenini, kutokana na viwanja vyake kuwa kwenye ukarabati wa kuelekea maandalizi ya Fainali za mwakani za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023).

"Tunatakiwa tuwe na tahadhari kwa sababu nimeona katika michuano hii kila timu inashinda nyumbani, ukiangalia RS Berkane na sisi tumeshinda mechi mbili nyumbani, ni sisi pekee mpaka sasa ndiyo tuliopata angalau pointi moja ugenini. Lengo ni kutaka kushinda ugenini ili kufuzu, tutajitahidi kufanya hivyo, lakini kama itashindikana, basi tutafuzu kwenye mechi yetu ya mwisho dhidi ya US Gendamerie," alisema Pablo.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanatarajia mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu hiyo ni mechi ya mwisho ya nyumbani kwa Asec Mimosas, hivyo watahitaji kushinda ili kujiweka katika nafasi ya kusonga mbele.

"Inaonekana timu hiyo inakuwa hatari zaidi inapocheza kwenye uwanja huo kwa sababu imeshinda mechi zote mbili, lakini sisi tuko kwenye kampeni ya kushinda ugenini, safari hii tunataka kufuzu robo fainali tukiwa katika ardhi ya ugenini, siku zote Simba hushinda mechi ngumu na kuishangaza Afrika," alisema meneja huyo.

# YANGA, KMC FC MAWINDONI

### ●●●Nabi afunguka anakutana na wapinzani walioimarika tofauti na...

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ni kauli ya makocha wa timu mbili kati ya vinara, Yanga na KMC FC zinazotarajia kukutana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kupata pointi tatu na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC FC katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, uliochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani kutokana na mabadilko ya benchi la ufundi waliyofanya wapinzani wao tofauti na walivyocheza katika mzunguko wa kwanza.

Nabi alisema Yanga inakabiliwa na mechi tatu ngumu ikiwamo ya leo huku nyingine zikiwa ni dhidi ya Azam FC na baadaye watakapokutana na watani zao, Simba ambayo ni dabi kubwa kwa Afrika.

"Maandalizi kuelekea mechi yetu dhidi ya KMC FC yanaendelea vizuri, wapinzani wetu wana timu nzuri na hatutaingia uwanjani tukiwa na akili ya kwamba tuliwafunga katika mechi iliyopita,".

"Tunaenda uwanjani tukiwa tunaanza moja, tunakwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo kwa sababu kuna baadhi ya wachezaji wangu wamerejea kikosini akiwamo, Salum Abubakar (Sure Boy) na Chiko Ushindi," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza katika mchezo huo wachezaji mbalimbali akiwamo Yacouba Songne ambaye yeye atakaa nje ya uwanja hadi Juni mwaka huu, Saido Ntibanzokiza, Khalid Aucho na Jesus Moloko.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally alisema timu yake inawaheshimu Yanga ambao wana timu nzuri lakini pia hata ukiangalia mchezaji mmoja mmoja utabaini wana viwango vya juu.

Ahmad alisema wamefanya maboresho katika idara zote kwenye kikosi chao, hivyo anaamini wachezaji wake wana uwezo wa kupata matokeo chanya.

"Ukiangalia Yanga ni wazuri kila sehemu, wanapopoteza mpira wanakuwa nyuma wote na wakipata mpira wanashambulia basi wanakuwa zaidi ya wachezaji saba kutafuta ushindi, tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kulingana na maandalizi tuliyowapa wachezaji wetu," alisema Ahmad.

Sudi Dondora ambaye amewakilisha wachezaji wa KMC kuelekea mchezo huo alisema licha ya kuwaheshimu Yanga, wao wamejiandaa vizuri kuhakikisha hawapotezi tena mchezo huo wa marudiano katika msimu huu.

"Tunawaheshimu Yanga kutokana na ubora wao lakini tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo mazuri na hatimaye kufikia malengo yetu," alisema Dondora.

Nyota huyo aliongeza wamejiandaa kuwapunguza kasi vinara hao na kuweka rekodi ya kwanza ya kuwafunga katika msimu huu unaoelekea ukingoni.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 ikiwa na pointi 45 ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 37 wakati KMC iliyoko katika nafasi ya saba ina pointi 22.

Ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itasimama kupisha mechi za Timu ya Taifa (Taifa Stars), itakayocheza dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan na itaendelea tena kuanzia Aprili Mosi, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >